# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

**MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN,**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024:**

## YALIYOMO

1. UTANGULIZI ....................................................................1
2. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022- MACHI 2023 ........................2
2.1 Ukusanyaji wa Mapato ................................................3
2.2 Mafanikio ya Ukusanyaji wa Mapato ............................4
2.3 Changamoto za Ukusanyaji wa Mapato .........................4
2.4 Matumizi ya Wizara kwa kipindi cha Julai 2022 – Machi 2023 .................................................................4
3. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022-MACHI 2023 ....................................5
3.1 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda ...........................................5
3.2 Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali ..........................................................13
3.3 Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara...18
4. UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 – MACHI 2023 ............31
4.1 Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Parks)........................................31
4.2 Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo wadogo, Wadogo, Wakati na Wakubwa (Khalifa Fund)..32
4.3 Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar .................................................34
4.4 Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ...............................................................34
4.5 Mradi wa Kuongeza Ushindani kwa Wazalishaji Wadogo na Kuanzisha Msingi wa Usafirishaji kwa Kuzingatia Fursa za

Biashara na Umoja wa Ulaya (EU) ....................................38
5. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022-MACHI 2023 ....................................41
5.1 Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na Vya Kati (SMIDA) ....................................41
5.2 Wakala wa Usajili Biashara na Mali (BPRA)....................................44
5.3 Wakala Wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) ....................................46
5.4 Tume Ya Ushindani Halali Wa Kibiashara Na Kumlinda Mtumiaji (ZFCC) ....................................47
5.5 Baraza La Ushindani Halali Wa Biashara Zanzibar (ZFTC) ....................................50
5.6 Baraza La Udhibiti Wa Mfumo Wa Utoaji Leseni Zanzibar (BLRC) ....................................51
5.7 Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ....................................53
5.8 Baraza la Taifa La Biashara (ZNBC)....................................55
5.9 Shirika la Biashara La Taifa (ZSTC) ....................................57
5.10 Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) ....................................61
6. MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024....................................63
6.1 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2023/2024....................................63
6.2 Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2023/2024 ....................................72
7. MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024: ....................................77
7.1 Mapato ya Serikali....................................77
7.2 Matumizi ....................................79
8. SHUKRANI: ....................................80
9. HITIMISHO: ....................................81
10. VIAMBATANISHO ....................................82

# HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN, KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024:

## 1. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema pamoja na kutuwezesha kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani pamoja na kusherehekea sikukuu ya iddil fitri katika hali ya salama na amani. Aidha, namshukuru kwa kutuwezesha kufika katika Baraza lako hili leo ili kuendelea kutekeleza majukumu ya kujenga nchi yetu katika kipindi hiki cha awamu ya nane ya uongozi hapa Zanzibar.

2. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake imara uliojaa hekima na busara na wenye azma kubwa ya kuiletea Zanzibar maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, namshukuru kwa kuendelea kuniamini kwa kunipa dhamana ya kusimamia sekta ya biashara na viwanda. Vile vile, nawashukuru kwa dhati Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa usimamizi na miongozo wanayotupatia katika kuziendeleza sekta hizi.

3. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza kwa kuliongoza vyema na kwa umahiri mkubwa Baraza letu la Wawakilishi. Vile vile, ninawapongeza Wenyeviti wa kamati mbali mbali na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa ushauri na maelekezo wanayotupatia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee naishukuru Kamati ya sekta ya Kilimo, Biashara, na Utalii inayoongozwa na Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi pamoja na wajumbe wake wote kwa kuchambua mapendekezo ya awali ya bajeti hii ya mwaka 2023 -2024 na hatimae kuridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa kujadiliwa na kuidhinishwa.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwapongeza wafanyabiashara na wazalishaji wote wa bidhaa hapa nchini kwa kuwajali wananchi wa Zanzibar wakati wa Mfungo wa ramadhani kwa kuridhia wito wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipowaomba kutopandisha bei za vyakula ili wananchi wapate unafuu wakati wakitekeleza ibada ya funga. Hakika wafanyabiashara na wazalishaji wa bidhaa hususan wakulima wameonesha kumuunga mkono Rais wetu na hivyo wanastahili pongezi kubwa sana. Kwa niaba ya Serikali na Wizara yangu tunawapongeza sana kwa uungwana wao.

6. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani zangu za pekee zimuendee Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Ali Khamis Juma kwa kuwa viungo muhimu kati yangu na watumishi wengine na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi katika kuhakikisha malengo ya Wizara yanafikiwa. Pia, nawashukuru kwa dhati Wakurugenzi na viongozi wote wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa juhudi zao kubwa za kuchapa kazi pamoja na mashirikiano makubwa wanayonipa yaliyosaidia katika utekelezaji mzuri wa majukumu yangu.

7. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya shukrani na maelezo hayo ya awali, naanza hotuba hii kwa kuwasilisha utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023, na hatimae nitawasilisha mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

## 2. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022-MACHI 2023

### 2.1 Ukusanyaji wa Mapato

8. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 4.60** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato. Kwa kipindi cha miezi tisa Wizara ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 3.47,** hadi kufikia 31 Machi, 2023 jumla ya **Shilingi bilioni 2.86**

zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni sawa na asilimia **83** ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi cha miezi tisa. Mchanganuo wa mapato unaonekana katika **Kiambatisho Namba 1.**

### 2.2 Mafanikio ya Ukusanyaji wa Mapato

9. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kupitia Idara na Taasisi zake imeweza kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato kwa sababu ya kufunguka kwa shughuli za kibiashara, kuongezeka usajili wa vyombo vya moto na upimaji wa mafuta yanayoingia nchini.

### 2.3 Changamoto za Ukusanyaji wa Mapato

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa changamoto katika suala la ukusanyaji mapato ni pamoja na Ukosefu wa wataalamu wa kutosha na vitendea kazi katika taasisi zikiwemo ZBS, ZAWEMA, BPRA na ZFCC na Baadhi ya maeneo kukodishwa muda mrefu ambapo kodi ya maeneo hayo imeshalipwa.

### 2.4 Matumizi ya Wizara kwa kipindi cha Julai 2022 – Machi 2023

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi bilioni 26.37** kwa ajili ya

kutekeleza programu zake. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 Wizara ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 22.4** ambapo, jumla ya **Shilingi bilioni 8.32** zilizopatikana sawa na asilimia **37** makadirio. Fedha zilizopatikana Kwa kipindi cha miezi tisa ni sawa na asilimia **31** ya makisio ya mwaka. Kati ya fedha hizo jumla ya **Shilingi bilioni 5.15** ziliingizwa kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 1.39** kwa ajili ya kazi za maendeleo na **Shilingi milioni 1.7** kwa kazi za kawaida. Mchanganuo wa matumizi hayo unaonekana katika **Kiambatisho Namba 2.**

## 3. Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa Kipindi cha Julai 2022-Machi 2023

12. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia program kuu tatu ambazo ni Programu kuu ya uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; Programu kuu ya maendeleo ya viwanda na ujasiriamali na Programu kuu ya ukuzaji na uendelezaji wa biashara. Utekelezaji wa program hizo ni kama ifuatavyo: -

### 3.1 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

13. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

imeundwa na Programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji wa Wizara; Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti; na Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba. Program hii ilipangiwa matumizi ya Shilingi bilioni 2.98 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 2.34** hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi bilioni 2.33** sawa na asilimia **99** zimeingizwa kwa ajili ya matumizi ya mishahara na kazi nyengine za uendeshaji. Utekelezaji wa huduma zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo: -

**Programu Ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara:**

**14.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni pamoja na huduma ya Ununuzi wa Vifaa vya Ofisi na Usafiri; huduma ya Usimamizi wa Rasilimali Watu na Huduma kwa Ujumla pamoja na Kuratibu Mikutano ya Majadiliano ya Kibiashara na Viwanda ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya Shilingi bilioni 1.71 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu hii ndogo ilipangiwa **Shilingi bilioni 1.31** hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi bilioni 1.34** sawa na asilimia **102** zimeingiziwa kwa ajili ya mishahara na kazi

nyengine za uendeshaji. Huduma za Program ndogo ya Utawala na Uendeshaji zilitekelezwa kama ifuatavyo: -

***Usimamizi wa Rasilimali Watu na Huduma kwa Ujumla***

15. **Mheshimiwa Spika** Wizara imefanikiwa kutekeleza huduma hii kwa:

a) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 7 katika fani ya Rasilimali watu, Uchumi, Uhandisi wa Viwanda, Uongozi wa Biashara na Usimamizi wa Kumbukumbu. Aidha, wafanyakazi 52 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi yanayohusiana na Ofisi Mtandao (E-Office), uwekaji kumbukumbu na utunzaji wa siri za Ofisi.

b) Kuwapatia Wafanyakazi 65 likizo, kati ya hao wafanyakazi 43 likizo la kawaida, wafanyakazi 21 likizo la dharura na mfanyakazi mmoja (1) likizo ya bila malipo. Aidha, mfanyakazi 1 amestaafu kazi kwa kutimia umri wa lazima.

c) Kufanyika kwa vikao vya Bodi ya zabuni vilivyopitisha Mpango wa Manunuzi wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na kujadili mambo mbalimbali yakiwemo ununuzi wa huduma za ofisi na uendelezaji wa maeneo ya viwanda na Maendeleo ya Ujenzi wa uwanja wa maonesho Nyamanzi.

d) Kuandaa ripoti ya mwaka 2021/2022 ya ukaguzi wa Mapato na Matumizi.

e) Kufanya malipo ya huduma ya kodi ya jengo, huduma za usafi na matengenezo ya magari na ofisi na malipo ya umeme na maji.

***Huduma ya Ununuzi wa Vifaa vya Ofisi***

16. **Mheshimiwa Spika** kupitia huduma hii Wizara imefanya manunuzi ya mafuta lita 4,200 za petrol na lita 650 za dizeli, Bendera tisa, ununuzi wa mafaili 20, magamba (binding cover), wino (Toner 59A, 117A) na Peni boksi 2.

***Uratibu wa Mikutano ya Majadiliano ya Kibiashara na Viwanda ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa***

**Mheshimiwa Spika** kupitia huduma hii Wizara imefanikiwa kuratibu ushiriki wa viongozi katika mikutano semina na makongamano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yanayohusiana na sekta za biashara na viwanda zilizofanyika nchini Ivory coast, Switzerland, Botswana na Tanzania.

**Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara**

17. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii ndogo imeendelea kutekeleza majukumu yake

ya kutayarisha, kuchambua na kutathmini utekelezaji wa mipango na malengo maalum ya Wizara. Huduma ambazo zimesimamiwa na Programu hii ndogo ni Uandaaji sera na Uibuaji wa Tafiti za Wizara, Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Wizara na Usimamizi wa Takwimu za Biashara na Viwanda. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya **Shilingi milioni 522.11** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu hii ndogo ilipangiwa **Shilingi milioni 439.70** hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi milioni 341.13** sawa na asilimia **78** zimeingiziwa kwa ajili ya mishahara na kazi nyengine za uratibu.

***Uandaaji wa Sera na Uibuaji Tafiti za Wizara***

**18.** **Mheshimiwa Spika**, kupitia huduma hii Wizara imekamilisha mapendekezo ya tafiti (Research Proposal) ya Nakisi ya Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara; Mpango wa Utafiti wa Wizara 2022-2026 wa muda wa miaka mitano wa Wizara; na Rasimu ya sheria ya Leseni imekamilika na hatua inayofuata ni kuiwasilisha kwa wadau kwa ajili ya maoni na baadae serikalini.

***Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Wizara***

**19.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia huduma hii Wizara imekamilisha uandaaji wa taarifa za utekelezaji kwa kila robo mwaka na kuziwasilisha katika Kamati ya Biashara,

Kilimo na Utalii pamoja na taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023; na uandaaji wa bajeti 2023/2024. Wizara pia imekamilisha uandaaji wa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo mwaka na kuziwasilisha Tume ya Mipango. Aidha, imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya Wizara ikiwemo Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi. Vile vile Wizara imewapatia mafunzo ya uandaaji wa Bajeti, maafisa Mipango na wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizopo chini ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

***Usimamizi wa Takwimu za Biashara***

**20. Mheshimiwa Spika,** kupitia huduma hii Wizara imekamilisha ukusanyaji wa taarifa za takwimu za Biashara kwa robo mwaka na ripoti ya taarifa hiyo imeandaliwa na kuchapishwa sambamba na kuziwasilisha kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Pia Wizara imetoa mafunzo ya mbinu na zana zinazotumika katika ukusanyaji wa takwimu za Biashara na Viwanda kwa Maafisa Takwimu wa Idara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

**Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba**

**21. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kutekeleza na kusimamia huduma za uratibu wa shughuli za Wizara ya

Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa upande wa Pemba. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya Shilingi milioni 745.37 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kati ya fedha hizo **Shilingi milioni 225.48** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi milioni 519.89** kwa ajili ya mishahara. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu hii ndogo ilipangiwa **Shilingi milioni 590.03** hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi milioni 645.23** sawa na asilimia **109** zimeingiziwa kwa ajili ya mishahara na kazi nyengine za uratibu na uendeshaji.

22. **Mheshimiwa Spika,** kupitia huduma hii ya ***Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba,*** ofisi kuu inatekeleza huduma zilizopo katika program ndogo za Wizara, kama zifuatazo: -

    i. Imefanya utafiti mdogo kwenye zao la Asali ili kupata Takwimu sahihi ya Wafanyabiashara wanaojishughulisha na bidhaa hii kwa Wilaya ya Chake chake ambapo jumla ya wadau 163 walifikiwa. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kwamba asali zaidi ya lita 2,419 zinazalishwa kwa Wilaya ya Chake chake;

    ii. Imetembelea vikundi 41 vya wajasiriamali na kuandaa mikutano mitano (5) kwa lengo la kusikiliza changamoto zao na kuweza kuzitatua katika Wilaya zote za Pemba, kati ya vikundi hivyo, vikundi kumi na sita (16) vilipatiwa mafunzo ya utengenezaji

(usarifu) wa bidhaa kwa kutumia mwani kwa bidhaa ya Sabuni, loshani, mafuta ya nywele, mafuta ya kujipaka, Juisi pamoja na Jamu.

iii. Imeratibu ushiriki wa vikundi kumi na tatu (13) katika maonesho ya saba saba Tanzania Bara na Tamasha la Biashara la Zanzibar;

iv. Imeandaa mikutano mitatu ya wadau wa sekta ya biashara wakiwemo Waingizaji wa bidhaa kutoka nje, Wasafirishaji wa bidhaa, wafanyabiashara wa mitumba, sokoni pamoja na Taasisi na Jumuiya zinazohusiana masuala ya biashara.

v. Imewapatia mafunzo ya awali ya Utumishi wa Umma wafanyakazi saba (7) juu ya namna ya kujua sheria na kanuni za kiutumishi katika kutekeleza majukumu yao. Vile vile, imeandaa vikao viwili (2) kwa wafanyakazi vya kujikinga na magojwa ya UKIMWI pamoja na Udhalilishaji na Unyanyasaji wa Kijinsia kwa jamii ili kujenga uimara wa Afya zao. Aidha imewapatia likizo za kawaida wafanyakazi ishirini na sita (26);

vi. Imefanya ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi, ununuzi wa huduma za umeme, ulipaji wa gharama za maji na mawasiliano, ununuzi wa mafuta na kutoa huduma ya usafiri kwa maafisa wa Wizara kwa ajili ya kufanikisha majukumu ya Wizara.

### 3.2 Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali

23. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda (DID) na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (SMIDA). Programu hii inajumuisha Programu ndogo mbili ambazo ni Ukuzaji Viwanda na Maendeleo ya Wajasiriamali. Program hii kuu ilipangiwa jumla ya Shilingi bilioni 13.70 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu hii ilipangiwa Shilingi bilioni 12.07 hadi kufikia Machi 2023, jumla ya Shilingi bilioni 1.53 sawa na asilimia 13 zimeingiziwa kwa ajili ya utekelezaji wa program hii. Program ndogo hizo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo: -

#### Programu Ndogo ya Ukuzaji Viwanda

24. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji wa Viwanda inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda (DID) ina jukumu la kutoa huduma ya kuimarisha sekta ya viwanda. Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 3.28** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 3.12** ambazo hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi bilioni 1.13** sawa na asilimia 39 zimeingiziwa kwa ajili ya mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyenginezo.

25. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia huduma ya ***Uimarishaji wa Sekta ya Viwanda*** katika ukuzaji na uboreshaji wa mazingira ya viwanda imepelekea kuongezeka kwa Mchango wa Viwanda katika pato la Taifa. Mchango huo umeendelea kuimarika kutoka asilimia **19** mwaka 2021 hadi kufikia asilimia **19.4** mwaka 2022 hii ni sawa na ongezeko la asilimia **0.4** ambapo sekta ya uzalishaji Viwandani ilichangia asilimia **8.1** kutoka asilimia 7 mwaka 2021. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika vinywaji (beverages), mabekari na viwanda vya vitambaa (garments).

26. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha nguo cha Basra Textile Mills Limited Kilichopo Chumbuni kinaendelea na uzalishaji wa bidhaa za vitenge na khanga. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia mwezi Machi 2023 kiwanda kimeweza kuzalisha mita 18,410,677.75 za vitenge na mita 1,301,460 za khanga ambapo uzalishaji wa vitenge umeongezeka kwa Zaidi ya mita 3,909,936 kutoka mita 14,500,741 za vitenge zilizozalishwa kwa mwaka 2021-2022. Aidha vitenge na khanga hizo zimeweza kuingia katika masoko ya nchi za Afrika Mashariki na SADC. Kiwanda hicho kwa sasa kimeweza kuajiri jumla ya wafanyakazi 314.

27. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Zanzibar Milling Corporation (ZMCL) kimezalisha jumla ya tani 45,229.745 za unga wa ngano, sawa na asilimia 37.7 ya uwezo wa kiwanda wa mwaka wa fedha 2022/2023 wa kuzalisha tani

119,880. Uzalishaji huo mdogo umetokana na kusimamisha uzalishaji mara kwa mara kutokana na shughuli za ujenzi wa kiwanda hicho. Aidha kiwanda kimezalisha tani 13945.65 za pumba (bran) ambapo jumla ya tani 11,688 zimeuzwa nje ya nchi. Kiwanda hicho kimeajiri jumla ya wafanyakazi 200, ambapo wafanyakazi 137 ni wa kudumu na 63 ni wa muda.

28. **Mheshimiwa Spika,** shughuli nyengine zilizofanyika katika huduma hii ni: -

i. Kushiriki katika vikao vya majadiliano ya kitaifa na nchi za SADC kuhusu kuendeleza viwanda uliofanyika Dar es Salaam kwa ajili ya kuridhia itifaki ya kuendeleza viwanda. Pamoja na kushiriki katika kikao cha EAC kilichojadili hali ya viwanda vya nguo, ngozi, kuunganisha magari, matunda na mbogamboga;

ii. Kuratibu shughuli za Uanzishwaji wa Viwanda katika eneo la viwanda la Chamanangwe ambapo mpaka sasa Wizara imepokea maombi 6 ya wawekezaji na maombi 5 yameshapatiwa hati ikiwemo kiwanda cha kusarifu zao la mwani, kiwanda cha mabati, mafuta ya kula, chakula cha mifugo pamoja na chumvi.

iii. Kuratibu na kushiriki katika maonesho ya bidhaa za Viwanda vya ndani kwa kushirikiana na Mamlaka ya Biashara Tanzania (Tan Trade) pamoja na Idara ya Biashara yaliofanyika kuanzia tarehe 3 hadi 9 katika

Viwanja vya maonesho vya Mwalimu Nyerere, Dar es salaam. Viwanda 4 vilishiriki katika maonesho hayo ambavyo ni: - Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo; Kiwanda cha korosho (YY-TZ Agroprocessing ltd – zanzibar); Kiwanda cha nguo na viatu (Vikosi Vya Idara Maalum - SMZ); Kiwanda cha uchongaji (Vocational Training Authority) na wajasiriamali kumi na mbili (12) wenye viwanda vidogo vidogo;

iv. Kufanya utafiti mdogo (survey) ya viwanda ambapo jumla ya viwanda 78 vimetembelewa na taarifa zake zimekusanywa zinazojumuisha aina za viwanda, uzalishaji, masoko na changamoto zake

v. Wizara imefanya mkutano na wadau wa viwanda pamoja na baraza la uzalishaji (MCZ) kwa ajili ya kupata maoni ya changamoto za kiviwanda. Baadhi ya changamoto zimeshafanyiwa kazi ni pamoja na kupunguza baadhi ya tozo ambapo, ZBS imepunguza tozo ya uchunguzi kwa wajasiriamali kutoka Tsh. 200,000 hadi Tsh. 50,000/- pamoja na kuondosha ada ya 'Custom Processing Fees' (CPF) kwa mizigo inayokwenda Tanzania Bara.

vi. Wizara imeanza kuhamasisha wawekezaji kutumia nishati mbadala ambapo mpaka sasa mwekezaji mmoja tayari amefanikiwa kutumia nishati mchanganyiko ya "Hybrid Source of Energy" yaani

umeme wa taifa na umeme unaotokana na nguvu za jua.

vii. Katika kuandaa sheria ya viwanda, Wizara imefanya majadiliano na BRELA ambayo inasimamia Sheria ya Taifa ya Usajili na leseni za viwanda, kwa vile suala la leseni za Viwanda na takwimu zake ni mambo ya Muungano. Majadiliano hayo yaligusia mapitio ya Sheria, muundo wa kitaasisi, uteuzi wa wajumbe pamoja na utaratibu wa utoaji wa leseni na mfumo.

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali**

**29. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda (DID) na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (SMIDA) kupitia huduma ya uratibu na utekelezaji wa sera ya MSME's na ukuzaji wa MSME's na Uendelezaji Ujasiriamali. Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ina jukumu la kuongeza mchango wa uzalishaji wa sekta ya ujasiriamali katika pato la Taifa. Program hii ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 10.43** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 8.95** hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi milioni 300.27** sawa na asilimia **3** zimeingiziwa kwa ajili ya mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida. Utekelezaji wa huduma hizo ulikuwa kama ifuatavyo: -

**30. Mheshimiwa Spika,** kupitia huduma ya Uratibu na utekelezaji wa Sera ya MSME's Wizara imetekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuchapisha vitabu 100 vya sera ya wajasiriamali wadogo wa wadogo, wadogo na wakati ili kuweza kuendelea na shughuli za uratibu wa wajasiriamali pamoja na kuwakuza ili kuleta tija na maendeleo kwa sekta hii;

ii. Kufanyika kwa kikao kimoja cha Kamati ya Mashauriano ya wajasiriamali ambapo wajumbe wa kikao hicho walihudhuria na kutoa maoni katika kufanikisha shughuli za ujasiriamali. Aidha, Wizara inaendelea na ufuatiliaji wa maazimio ya kikao hicho kwa ajili ya utekelezaji.

### 3.3 Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara

**31. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara, utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Biashara pamoja na taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Programu hii inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo ni Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji; Uwezeshaji Biashara; na Utengamano wa Biashara na ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 9.69** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 8.01** hadi kufikia Machi

2023, jumla ya **Shilingi bilioni 4.47** sawa na asilimia **46** zimeingiziwa kwa mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida. Aidha, Utekelezaji wa Program ndogo hizo ni kama ifuatavyo: -

**Programu Ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji**

**32. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM). Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha nafasi ya Zanzibar katika usafirishaji wa bidhaa katika Masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa. Huduma ambayo inasimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Kuongeza Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara.Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 4.96** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 4.20** hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi bilioni 1.00** sawa na asilimia **24** zimeingiziwa kwa ajili ya mishahara na kazi nyengine za kawaida.

**33. Mheshimiwa Spika,** Katika Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji nje imepelekea hali ya biashara kwa ujumla kuimarika na kuwa bora kwa kipindi cha mwaka 2022-2023, ambapo Zanzibar ilifanya biashara yenye thamani ya **TZS bilioni 1,439.4** ikilinganishwa na **TZS bilioni 1,124.3** mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia **28.0**,

Kama inavyoonekana katika **kiambatanisho Nambari 3.** Biashara hiyo ilikuwa ni usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya Zanzibar na uagiziaji wa bidhaa kuingia Zanzibar. Bidhaa zilizosafirishwa nchi za nje ni pamoja na karafuu, mwani na mazao ya baharini, vitenge na khanga.

34. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022-2023 Zanzibar ilisafirisha nje bidhaa zenye thamani ya **TZS bilioni 180.37.** Kiwango hicho cha usafirishaji ni sawa na ongezeko la asilimia **15.9** ikilinganishwa na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya **TZS bilioni 155.67** uliofanyika kipindi cha mwaka 2021. Bidhaa zilisafirishwa katika masoko ya Singapore, na Nchi za Falme za Kiarabu (UAE), Indonesia, India na Denmark.

35. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uagiziaji bidhaa, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya **TZS bilioni 1,258.98** kwa mwaka 2022 (kama inavyooneshwa kwenye mchoro **Kiambatanisho Namba 4**). ikilinganishwa na uagiziaji wa **TZS bilioni 968.64** kwa mwaka 2021. Bidhaa ambazo Zanzibar imeagiza kutoka nchi za nje ni pamoja na Mafuta, Bidhaa za Viwandani, vyombo vya usafiri, bidhaa za nguo na bidhaa za chakula. Zanzibar inaagiza bidhaa kwa wingi kutoka nchi za Falme za Kiarabu, China, India na Pakistani, Brazil, Uturuki, na Vietnam.

36. **Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa usafirishaji Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kipindi cha mwaka

2022, Zanzibar ilisafirisha bidhaa kwenda Tanzania Bara zenye thamani ya **TZS bilioni 37.64,** ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya **TZS bilioni 33.99** zilizosafirishwa mwaka 2021. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2022, Zanzibar iliagizia kutoka Tanzania Bara bidhaa zenye thamani ya **TZS bilioni 375.80** ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya **TZS bilioni 288.26** kwa mwaka 2021.

37. **Mheshimiwa Spika;** Hali ya uwepo wa bidhaa muhimu za chakula hapa Zanzibar umeendelea kuridhisha na vyakula vyote vinaendelea kupatikana bila ya usumbufu nchini. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya Tani 99,971 za mchele, Tani 4,302 za sukari, Tani 5,687 za unga wa ngano na tani 84,839 za mafuta ya kula ziliingizwa Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani. Hatahivyo, uzalishaji wa ndani uliendelea kwa bidhaa za unga wa ngano ambao unazalishwa na kiwanda cha Zanzibar Milling kilichopo Mtoni. Takwimu zinaonesha jumla ya tani 41,720 za unga wa ngano na tani 6,796 za sukari zilizalishwa katika kiwanda cha Sukari kilichopo Mahonda kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023. Kama inavyoonekana katika **kiambatanisho namba 5.**

38. **Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa bei za bidhaa muhimu kama vile mchele, unga wa ngano pamoja na sukari katika soko la ndani zimekuwa zikiongezeka bei kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa hizo katika masoko

ya dunia. Wizara iliendelea na utaratibu wa kupanga bei elekezi na kusimamia bei hizo kwa lengo la kuleta unafuu wa bei kwa wananchi wa Zanzibar. Katika upangaji huo wa bei, Wizara ilishirikiana na makundi mbali mbali ikiwemo wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa nchini, Mamlaka za kodi, taasisi zinazotoa tozo kwa wafanyabiashara na mashirika ya meli ili kupata taarifa sahihi. Bei za bidhaa muhimu zinaonekana katika **kiambatanisho nambari 6.**

***Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara***

**39.** **Mheshimiwa Spika**, kupitia huduma hii Wizara imetekeleza shughuli zifuatazo:

i. Imeratibu ushiriki wa Zanzibar katika maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara (sabasaba) yaliyofanyika Dar es Salaam mwezi wa Julai 2022. Jumla ya washiriki 54 kutoka Zanzibar wameshiriki katika maonesho hayo. Miongoni mwa washiriki hao ni wajasiriamali 38, taasisi za Serikali 9 pamoja na Kampuni binafsi 7. Bidhaa ambazo zilionyeshwa na washiriki katika maonesho hayo ni pamoja na bidhaa za kusindika, kazi za mikono, nguo, vitenge, sabuni, dawa za asili, bidhaa za viungo (spices) na mafuta ya mimea. Aidha, huduma mbali mbali zilioneshwa zikiwemo huduma za usafiri (angani na baharini) pamoja na huduma za ukuzaji na usimamizi wa biashara na uwekezaji;

ii. Imeratibu ushiriki wa wajasiriamali wa Zanzibar katika Maonesho ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya Jua Kali/ Nguvu Kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji yaliyofanyika Disemba, 2022 nchini Uganda. Jumla ya wajasiriamali 22 kutoka Zanzibar wameshiriki katika maonesho hayo na kuonesha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar ambazo ni pamoja na sabuni, kazi za mikono na bidhaa za kusindika;

iii. Imeandaa Tamasha la 9 la Biashara la mwaka 2023 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka huu Tamasha hili lilijumuisha jumla ya washiriki 408 kati ya hao 78 ni Taasisi za Serikali, 23 kampuni kubwa, 307 ni wafanyabiashara na wajasiriamali. Miongoni mwa wafanyabiashara hao, washiriki 7 kutoka Uganda, 4 kutoka Burundi, 2 kutoka Kenya, na mshiriki 1 kutoka Zambia, 1 Misri, 1 Ghana na 1 India. Aidha, wizara ilipokea ujumbe maalum kutoka mkoa wa Njombe uliowakilishwa na uongozi wa Mkoa ambapo walipata fursa ya kutangaza bidhaa zao ikiwemo mbao, mbatata na parachichi kwa soko la Zanzibar.

Vile vile, kupitia Tamasha hilo, Wizara imeratibu na kuandaa siku maalum sita ambazo ni siku maalum ya MKURABITA; Ubunifu; Matumizi ya Mkaa Rafiki (STAMICO); Siku ya Bidhaa zinazozalishwa Zanzibar

(Made in Zanzibar); BATIKI na siku Maalum ya majadiliano baina ya Taasisi za Wizara za Biashara za SMZ na SMT. Lengo ni kuweza kuwakutanisha watumiaji, wazalishaji wa bidhaa pamoja na Taasisi zinaohusika na masuala ya biashara na uzalishaji kufanya majadiliano, kuibua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara na wazalishaji, na kutoa mapendekezo katika kuimarisha na kukuza sekta ya biashara na uzalishaji nchini;

iv. Imeandaa mikutano ya wafanyabiashara na wazalishaji wa ndani kwa lengo la kushajiisha wamiliki na wafanyabiashara kununua bidhaa zilizozalishwa nchini. Matokeo ya mikutano hiyo, imeonesha matumaini kwa wamiliki kununua bidhaa za wazalishaji nchini kwa kuzingatia ubora, wingi na bei za bidhaa hizo.

**Programu Ndogo ya Uwezeshaji Biashara**

**40. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uwezeshaji Biashara inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko pamoja na taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Biashara. Programu hii ndogo ina lengo kuharakisha utoaji wa bidhaa na kuboresha taratibu za utoaji mizigo pamoja na kupunguza taratibu, gharama na muda wa usafirishaji na uingizaji bidhaa nchini. Huduma ambazo zinasimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Uimarishaji na

Uwezeshaji Biashara; Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali; Uimarishaji wa Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji; Usikilizaji na Utoaji wa Maamuzi ya Rufaa za Ushindani zinazotokana na Mamlaka za Uthibiti; Uimarishaji wa Majadiliano ya Kibiashara Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Usimamizi wa Mamlaka zinazotoa Leseni; Uandaaji wa Viwango na Tathmini ya Ubora; na Utoaji Huduma ya Ulinganishi na Matumizi sahihi ya Vipimo.

Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 4.63** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 3.73** hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi bilioni 3.45** sawa na asilimia **93** zimeingiziwa kwa ajili ya mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida. Utekelezaji wa huduma ya program ndogo hii ni kama ifuatavyo;

***Uimarishaji na Uwezeshaji Biashara***

**41. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa huduma hii ya Uimarishaji na Uwezeshaji wa Biashara ni kama ifuatavyo:

i. Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango pamoja na MKURABITA imefanya ukarabati wa Kituo Jumuishi cha Urasimishaji na uendelezaji biashara katika Wilaya ya Kaskazini A Unguja ambapo kituo hicho kinaendelea kutoa huduma kwa wafanyabiashara.

Kupitia kituo hicho, jumla ya wafanyabiashara 983 waliopo katika Wilaya ya Kaskazini A wamepatiwa leseni za uendeshaji wa Biashara, na wafanyabiashara 24 wamesajiliwa katika mfumo wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA);

ii. Wizara imekamilisha ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Urasimishaji na uendelezaji wa biashara katika Wilaya ya Chake Chake, Pemba. Kituo hicho kitawasaidia wafanyabiashara wadogo kupata huduma za usajili wa majina ya biashara, huduma za leseni ya biashara pamoja na huduma nyengine za Biashara. Kituo kinatarajia kuanza kazi mwaka mpya wa Fedha 2023/2024.

iii. Wizara imefanya ufuatiliaji na tathmini ya wafanyabiashara wadogo wadogo 165 waliopewa mafunzo ya Urasimishaji kwa mwaka 2022 katika Wilaya ya Micheweni, Pemba. Ufuatiliaji huo umebaini jumla ya wafanyabiashara 69 tayari wameshafanya usajili wa biashara zao na wanaendelea kufanya biashara katika mfumo ulio rasmi. Miongoni mwa wafanyabiashara hao 21 wamefanya usajili wa BPRA na 48 wamepatiwa leseni za kuendesha Biashara;

iv. Wizara imefanya vikao na wafanyabiashara wanaosafirisha na kuingiza bidhaa nchini ili kujadili kero na malalamiko yao katika ufanyaji wa biashara

na vikwazo wanavyokumbana navyo katika harakati zao za kibiashara. Miongoni mwa wafanyabiashara waliokutanishwa ni wanaojihusisha na biashara ya dagaa; wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa kutoka Guangzho-China; wanaoingiza na kusafirisha mchele na sukari pamoja na wafanyabiashara wa chuma chakavu;

v. Wizara imefanya kazi za ukaguzi katika maeneo ya wafanyabiashara ambao wanafanya biashara ya kuingiza na kusafirisha bidhaa kutoka Zanzibar kwenda nje ya nchi. Kupitia ukaguzi huo, wafanyabiashara 164 wamepatiwa hati za usajili wa biashara (Import /Export Registration Certificate) kwa kipindi hiki;

vi. Wizara imefanya ukaguzi katika kampuni zinazomilikiwa na wageni na zilizoajiri wafanyakazi wa kigeni kwa lengo la kuweza kujua shughuli zinazofanywa na kampuni hizo kabla ya kuwaombea vibali vya ukaazi na kufanya kazi nchini. Kwa kipindi cha Julai – Machi, jumla ya wafanyabiashara wa kigeni 107 wameombewa vibali vya kufanyakazi nchini, kati ya maombi hayo, maombi 10 yamekataliwa kwa kutokidhi masharti ya uhalali wa biashara zao kulingana na sheria za nchi;

vii. Wizara imeandaa kanuni tano zinazohusiana na biashara kwa lengo la kuweka utaratibu mzuri wa

usimamizi wa masuala ya biashara ya bidhaa na huduma nchini. Kanuni hizo ni Kanuni ya Bidhaa Zinazodhibitiwa; Kanuni ya Mauziano kwa Njia ya Mkopo; Kanuni ya Biashara ya bidhaa Chakavu; Kanuni ya Usimamizi na Uendeshaji wa Maonesho na Kanuni ya Ufanyaji Biashara;

**Programu Ndogo ya Utengamano wa Kibiashara**

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utengamano wa Kibiashara inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM). Programu hii ndogo ina lengo kuimarisha biashara inayopelekea upanuzi wa soko na kuongeza biashara baina ya nchi na nchi. Huduma ambayo inasimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Uimarishaji wa Utengamano wa Kibiashara.

Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 105.4** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 – Machi 2023 programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi milioni 82.74,** hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi milioni 7.45** sawa na asilimia **9** zimeingiziwa kwa ajili ya kazi za kawaida. Utekelezaji wa huduma za program ndogo hii ni kama ifuatavyo;

***Uimarishaji wa Utengamano wa Kibiashara***

43. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu na kushiriki mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa inayohusiana na masuala ya biashara. Mikutano hiyo ni pamoja na:

i. Mkutano wa majadiliano ya kupitia Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE);
ii. Vikao vya majadiliano ya Mkakati wa Biashara ya Mtandao wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki pamoja na vikao vya majadiliano ya kuanzisha Mfumo wa Pamoja wa Uondoshaji wa Shehena Maeneo ya Forodha. Mfumo huo utarahisisha utendaji kazi na kuongeza mapato ya Serikali kupitia bandari;
iii. Vikao vya majadiliano ya Sera ya Biashara ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Umoja wa Nchi za Jumuiya ya Ulaya;
iv. Majadiliano ya maendeleo ya ufanyaji biashara katika eneo huru la biashara barani Afrika (AfCFTA);
v. Vikao vya itifaki ya biashara ya huduma Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC);
vi. Vikao vya kujadili kuondosha vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiushuru (NTBs) na vikao vya urahisishaji biashara (Trade Facilitation);
vii. Vikao vya usimamiaji wa masuala ya TBT na SPS na vikao vya SADC kwa lengo la kurahisisha ufanyaji biashara katika soko la kikanda na Kimataifa.

**Mashirikiano na TanTrade**

44. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tan Trade) ambayo ni Taasisi ya Muungano imekua ikishirikiana kwa karibu na Wizara ya Biashara na

Maendeleo ya Viwanda katika kutekeleza majukumu yake kwa upande wa Zanzibar yakiwemo ya kuendeleza na kukuza biashara ya ndani na nje ya Nchi. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Mamlaka kupitia ofisi yake ya Zanzibar imefanya juhudi za uendelezaji na ukuzaji wa Biashara Zanzibar ili kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar zinapata masoko na zinaendelezwa. Mamlaka imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

a) Kushiriki katika uratibu wa Tamasha la tisa (9) la Biashara ambapo Mamlaka iliratibu Kliniki ya Biashara iliyojumuisha Taasisi wezeshi 16, na jumla ya changamoto 298 zilipokelewa na kutatuliwa; na

b) Kufanya ziara kwa Taasisi tatu (3) ikiwemo ZAFICO, Wakala wa Uchumi na Uwezeshaji Zanzibar (ZEEA) na Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO) kwa lengo la Kujenga mashirikiano ya kikazi katika kutatua changamoto za wajasiriamali ikiwemo, kushirikiana katika upatikanaji wa Rasilimali fedha na utaalamu pamoja na kufanya tafiti mbalimbali za kimasoko.

c) Mamlaka pia ilifanikiwa kuratibu ujio wa ujumbe wa Serikali ya Korea Kusini uliokutana na wawakilishi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kupitia mkutano huo pande mbili zilikubaliana; kukuza biashara na Uchumi wa Bluu kwa kuhakikisha Tanzania inapata masoko ya uhakika nchini Korea; kushiriki na kuandaa Expo ikiwemo Busan Expo inayotarajiwa kufanyika mwaka 2030 na kubadilishana uzoefu;

45. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Mamlaka imeendelea kufanya jitihada ya kuimarisha na kuendeleza ufanisi wa utendaji wa majukumu kwa kuongeza wafanyakazi watano (5) kutoka wafanyakazi wawili (2) waliokuwepo awali, kwa ofisi ya Zanzibar.

## 4. Utekelezaji wa Miradi Inayosimamiwa na Wizara Kwa Kipindi cha Julai 2022 – Machi 2023

### 4.1 Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Parks)

46. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuanzisha maeneo tengefu ya viwanda ili kuweza kujenga mazingira wezeshi ya uwekezaji wa viwanda Zanzibar. Sambamba na kuwavutia wawekezaji wa viwanda kuwekeza katika maeneo hayo, lengo pia kuongeza ajira na mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mradi huu ulipangiwa jumla ta **Shilingi bilioni 2.5,** hadi kufikia Machi 2023 mradi huu umeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 578.4** sawa na asilimia **23** ya makadirio kwa mwaka. Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

i. Wizara imekamilisha tathmini na kulipa fidia ya miti na mazao ya wananchi katika eneo tengefu la Viwanda Dunga Zuze ambapo jumla ya wananchi 34 wamelipwa fidia zao.

ii. Kukamilika kwa upimaji wa eneo (Topographic and Catastrophic Survey) ya eneo la Dunga na Chamanangwe, Mpango Mkuu (Master Plan) na Upembuzi yakinifu (Feasibility Study) wa matumizi ya Ardhi. Aidha, mzabuni wa kufanya kazi hiyo ameshapatikana ambae ni kampuni ya CRM iliyopo Dar es Salam na Wizara tayari imeshatia saini mkataba na kampuni hiyo kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa kazi;

**Vile vile,** miundombinu ya barabara tayari imeshajengwa katika eneo la Dunga kwa kiwango cha lami kutoka barabara kuu mpaka eneo la Viwanda, kwa upande wa umeme miundombinu tayari imeshawekwa katika eneo hilo.

### 4.2 Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo wadogo, Wadogo, Wakati na Wakubwa (Khalifa Fund)

**47. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mfuko wa Maendeleo (Khalifa Fund) kutoka Nchi za Falme za Kiarabu (UAE). Lengo la Mradi ni kuweza kuwasaidia wajasiriamali wadogo wadogo, wadogo na wa kati katika kujikwamua kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye gharama nafuu, mafunzo ya ujasiriamali pamoja na uboreshaji wa bidhaa wanazozizalisha ili ziweze kuongeza ushindani katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Kwa

mwaka wa fedha 2022/23, mradi ulipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 9.1,** kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 4.5** kutoka Serikalini ya Mapinduzi ya Zanzibar na **Shilingi bilioni 4.6** kutoka kwenye mfuko wa Khalifa Fund. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 mradi huu haukuingiziwa fedha.

48. **Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo mradi huu ulipokea fedha kutoka Nchi za Falme za Kiarabu mwishoni mwa mwaka 2021/2022 jumla ya **Shilingi bilioni 4.6,** fedha ambazo utekelezaji wake umeanza kutumika kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023. Mpaka kufikia Machi 2023 jumla ya **Shilingi bilioni 2.1** zimetumika sawa na asilimia **46** ya fedha za Khalifa Fund zilizoingia kwa kipindi hiki. Utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

i. Kuwapatia mikopo wajasiriamali 16, kati ya hao wajasiriamali 3 wadogo wadogo wenye bidhaa za utengenezaji Sabuni, Vinywaji laini na Mkandarasi wa Vifaa vya Ujenzi; Wajasiriamali 5 wadogo wenye bidhaa za tishu, chupa za maji, viungo, majani ya chai yenye viungo na kuku; na Wajasiriamali 8 wa kati wenye bidhaa za malighafi za Viwanda, hotel, Kuku, Mbao, Vifungashio, Kontena za alminiamu na Vifungashio vya mifuko ya karatasi;

### 4.3 Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar

49. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia mradi wa **Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar:** Wizara ya Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni 4.0** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi Milioni 811.9** sawa na asilimia **20** ya fedha zilizopangwa kwa kipindi hiki zimeingizwa katika kifungu hiki ambazo zilihaulishwa na kulipwa mzabuni wa vifaa vya maabara ya taasisi ya viwango (ZBS). Hata hivyo Utekelezaji katika mradi huu ni kama ifuatavyo:

   i. Kukamilika kwa michoro ya ujenzi wa eneo hilo pamoja na taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi;
   ii. Kukamilika kwa taratibu za zabuni ya ununuzi wa vifaa vya maonesho ikiwemo magazebo, Mashamiana na samani.
   iii. Kukamilika kwa usafishaji wa eneo la Maonesho na kuanza kwa ujenzi wa uzio, sehemu za kusimamisha magazebo, vyoo na jengo la utawala.

### 4.4 Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS)

50. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango (ZBS): Wizara imeweza kukamilisha maabara 4 ya Vimelea, Vifungashio, Nguo na Ngozi na

maabara ya Umeme pamoja na upatikanaji wa vifaa vya maabara hizo. Vifaa vilivyopokelewa na kufungwa ni pamoja na:

i. Vifaa vya maabara ya kupimia Ngozi na Vitambaa, vifaa vya maabara ya Chakula, vimelea na vifaa vya maabara ya Vifungashio. Aidha, Mafunzo kwa watendaji juu ya matumizi ya vifaa hivyo yameshafanyika kupitia kwa mzabuni aliyeshinda zabuni hiyo;
ii. Wizara imefanya ununuzi wa vifaa vya ICT vinavyohitajika pamoja na miundombinu inayohitajika na ZBS. Aidha, kampuni ya 'VASTECH COMPANY LTD, DAR -ES -SALAAM' imeshafanya tathmini ya ubora wa vifaa vilivyoletwa pamoja na kutoa ripoti ya kitaalamu. Ripoti imeonesha vifaa vyote vilivyofungwa katika Mradi vimekidhi mahitaji ya Mkataba;
iii. Mtambo wa kukagua vyombo vya moto (Automotive) ambapo Msambazaji 'Analyze (UK) Limited t/a Boston Garage Equipment' tayari amepewa kazi kwa ajili ya Ununuzi wa mtambo huo. Aidha, ZBS imeandaa BoQ na michoro ya ujenzi wa miundombinu itakayotumika kuweka vifaa vitakavyotumika, ujenzi wa eneo hilo tayari umeanza.

51. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022 – 2023 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imetekeleza progaramu tofauti kupitia washirika wa maendeleo. Kwa upande wa Trade Mark Afrika (TMA) Wizara imetekeleza yafuatayo: -

i. **Kufanya Tathmini ya Mfumo wa National online Business Service (NOBS):** Tathmini hiyo imefanyika kwa kuipitia mifumo ya taasisi 23 za usimamizi na udhibiti biashara. Taasisi zilizofanyiwa tathmini ni pamoja na Manispaa tatu (3), Halmashauri za Miji sita (6) na Wilaya Mbili (2) za Micheweni na Kusini, Mamlaka Saba (7) na Idara Tano (5). Aidha, ripoti ya tathmini hiyo imeshakamilika;

ii. **Kuandaa Mfumo wa Utoaji Huduma za Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS):** Wizara kwa kushirikiana na TMA imeandaa mfumo ambao utawezesha huduma zinazotolewa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) za uandaaji viwango na udhibiti wa ubora wa bidhaa na huduma kufanyika kielektroniki. Mfumo huo umepewa jina la "Viwango Jumuishi, Uhakiki wa Ubora, Ugezi na Upimaji" (Integrated Standards, Quality Assurance, Metrology and Testing, (iSQMT);

iii. **Kufanya tathmini ya Maabara za ZBS (Laboratory Need Assessment):** Katika kuanza kufanya kazi hii, Wizara imeandaa Hadidu Rejea (TORs) kwa ajili ya kuweka wazi maeneo yatakayofanyiwa mapitio na tayari zimeshawasilishwa TMA;

iv. **Kuandaa Jukwaa la Mafunzo ya Kielektroniki (Mtandaoni) kwa Sekta Binafsi na Wajasiriamali Zanzibar - (E-learning platform for Private Sector and SMEs Compliance in Zanzibar):** Lengo ni kuwawezesha Wajasiriamali

kupata elimu kupitia mtandao (online) ambapo Taasisi zote zinazohusika na masuala ya biashara zinashirikiana kutoa mafunzo kwa wajasiriamali. Wizara imeshaunda Kikosi kazi kwa ajili ya kuandaa modules zitakazoekwa kwenye mtandao. Hatua ya awali ya kukutana na wadau imefanyika na Hadidu Rejea zimeshaandaliwa kwa ajili ya kazi hiyo;

v. **Kuimarisha Majadiliano (dialogues) baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPD):** Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya wafanyabiashara (ZNCC) wameandaa Hadidu za Rejea (TORs) kwa ajili ya kuimarisha na kukuza majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Vilevile tathmini ya mahitaji ya kisera kwa sekta binafsi ilifanyika na uainishaji wa maeneo yenye vikwazo ulifanyika.

vi. **Kuimarisha vitendea kazi na mifumo ya kiteknolojia ya Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar (ZNBC):** Hadidu rejea zenye kuainisha idadi na aina ya vifaa vinavyohitajika imeandaliwa na mchakato wakupata Kampuni yakusambaza vifaa hivyo umeanza;

vii. **Kuwajengea uwezo watendaji wa Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Zanzibar (ZFCC):** Wizara kwa kushirikiana na TMA imeweza kuwapatia mafunzo watendaji wa taasisi hiyo hususani kwenye maeneo ya Bidhaa bandia (Counterfeit) na ushindani (Competition) ambapo Wataalamu kutoka Tume ya Ushindani ya

Tanzania bara waliongoza mafunzo hayo;

viii. **Kuandaa Mpango Mkakati (SP) ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:** Wizara kwa kushirikiana na TMA imekamilisha Mpango Mkakati wa Wizara (2023/24 – 2027/28) ambapo kazi hii ilifanyika kwa kushirikiana na Mshauri elekezi pamoja na wataalamu wa Wizara ya Biashara;

ix. **Kusaidia Wizara katika maswala ya kujikinga na Uviko 19:** Wizara ya Biashara imepokea vifaa mbalimbali kwa ajili ya kujikinga na tahadhari ya maradhi hayo. Vifaa hivyo ni pamoja na vitakasa mikono, vipima joto, barakoa, coverall na walk thermo scanner kwa ajili ya kuweka katika maeneo ya bandari na uwanja wa ndege. Wizara ya Biashara imekabidhi vifaa hivi kwa Wizara ya Afya kwa hatua za kuvitumia;

### 4.5 Mradi wa Kuongeza Ushindani kwa Wazalishaji Wadogo na Kuanzisha Msingi wa Usafirishaji kwa Kuzingatia Fursa za Biashara na Umoja wa Ulaya (EU)

**52. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kushirikiana na Taasisi ya Tafiti za kuondosha Umasikini (REPOA) kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) inasimamia na kuratibu utekelezaji wa mradi huu kwa taasisi za udhibiti ikiwemo Taasisi ya Viwango (ZBS), Mkemia Mkuu wa Serikali (CGCLA) pamoja na Wakala wa

Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA). Kwa mwaka wa fedha 2022 -2023 Wizara kupitia mradi huu imeweza kutekeleza shughuli ifuatayo:

i. Kutoa mafunzo kwa watendaji wa Taasisi za udhibiti ZBS, ZFDA na Mkemia Mkuu wa Serikali (CGCLA): Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na Mfumo wa usimamizi wa ubora (Quality Management System) kulingana na ISO 9001:2015, Mahitaji na Utekelezaji wa ISO/IEC 17025:2017, Uthibitishaji wa mbinu ya jumla na kipimo cha kutokuwa na uhakika (General Method Validation and measurement of uncertainties) na Tathmini ya ulinganifu (Conformity Assessment) kwa mujibu wa ISO/IEC 17065:2012.

**53. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022 – 2023, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya Tanzania Bara, Wadau wa maendeleo akiwemo Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Kuendeleza Biashara Duniani (WTO) kupitia mfuko wa Enhanced Integrated Framework – (EIF) iliendelea kutekeleza mradi wa **"Kuwaimarisha Wajasiriamali Wadogo wadogo, Wadogo na wa Kati Kuongeza Uwezo wa Uzalishaji na Ushindani Katika Masoko ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa Katika Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Dagaa na Mwani".** Kupitia mradi huu Wizara imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kukamilisha ununuzi wa Boti za kisasa 8 na mashine zake, vifaa vya kuzamia seti mbili mbili kwa kila boti, saa za mkononi, maboya na kuzikabidhi kwa vikundi vya Wajasiriamali wa ukulima wa Mwani Pemba katika maeneo ya Chokocho, Makangale, Tumbe na Wingwi. Vikundi vilivyopatiwa Boti hizo ni pamoja na Kikundi cha Ipo Sababu, Umwama, Yataka Moyo, Sebu Shari, Malengo Yetu, Seaweed Cooperative, Umoja Kazi na Wema Hauozi;

ii. Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) wamekamilisha utengenezaji wa Chanja 488 za kuanikia Dagaa ambazo zimekwisha kamilika na zinatarajiwa kufungwa katika eneo la Mradi wa Uchakataji wa Dagaa lililopo KAMA baada ya kukamilika kwa uwekaji sawa wa eneo la mradi;

iii. kufanya ununuzi wa mashine ya Ufungashaji na utiaji Nembo kwa bidhaa za Dagaa na Mwani kwa viwango tofauti ambapo kwa sasa Mashine hiyo imeshawasili nchini na inatarajiwa kukabidhiwa kwa Wizara mwezi Mei, 2023;

iv. imekamilisha rasimu ya Tafiti ya Faida na hasara ya sekta za kiuchumi katika kutekeleza soko huru la Afrika (Comprehensive Study on the Cost and Benefit Analysis on the implementation of the AfCTA in all sectors of economy in Tanzania); Rasimu ya Mpango wa utekelezaji wa soko huru la Afrika (The National AfCFTA Implementation Strategy), na Nyaraka ya Uchambuzi na Ushauri wa Kitaalamu kwa Majadiliano

yanayoendelea katika maeneo ya Uwekezaji, Mali Bunifu na Ushindani (Technical analytical paper and advice on the ongoing negotiations on the areas of Investment, Intellectual Property and Competition);

v. Wizara imewapatia mafunzo wajasiriamali 30 kwa upande wa Unguja na Pemba ya namna bora za Ufungashaji wa bidhaa, Utiaji Nembo, Branding, Uwekaji Kumbukumbu na Uandaaji wa Mpango wa Biashara. Vile vile, Wizara imetoa mafunzo ya uwelewa juu ya soko huru la Afrika na uwepo wa masoko ya Kikanda na Kimataifa kwa bidhaa za Dagaa na Mwani kwa Wafanyabiashara na Wajasiriamali 40 kwa Unguja na Pemba pamoja na fursa zilizopo katika masoko hayo.

vi. Wizara ya Biashara imewapatia watendaji wa Serikali na Sekta binafsi 40 Unguja na Pemba mafunzo ya Upitiaji (Review) Uchambuzi, Uandaaaji, na utekelezaji wa Sera za taasisi kwa lengo la kujenga ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao.

## 5. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022-MACHI 2023

### 5.1 Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na Vya Kati (SMIDA)

54. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (SMIDA) ambayo

utekelezaji wa majukumu yake kwa Wizara unaingia katika program kuu ya pili ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali kupitia program ndogo ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali. Kupitia program ndogo hii SMIDA ina lengo la kuwakuza na kuwaendeleza Wajasiriamali.

55. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 SMIDA kupitia huduma hii ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 10.36** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo ikiwemo fedha za Khalifa Fund. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 1.26** ni Ruzuku ya uendeshaji kutoka Serikali Kuu, hadi kufikia Machi, 2023 SMIDA imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 259.88** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini sawa na asilimia **20.6** ya makadirio ya mwaka.

56. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia huduma hii ya ***Ukuzaji wa MSME's na Uendelezaji wa Ujasiriamali*** SMIDA imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Imewapatia mafunzo Wajasiriamali 112 ya kuimarisha uweledi wa uzalishaji wa bidhaa, kati yao wanaume 69 na wanawake 43. Katika mafunzo hayo Wajasiriamali 30 wamepatiwa mafunzo ya kuongeza mnyororo wa thamani wa zao la chumvi; 22 mafunzo ya uanzishaji na uendelezaji wa makongano zikiwemo kongano za Mwani, Sabuni, Viungo, Mboga mboga na Matunda, Asali, Dagaa, Chumvi, Kuku na Mifugo ili kufikia uzalishaji wa mazao ya kimkakati katika Mikoa; 30

wamepatiwa mafunzo ya vigezo na sifa za bidhaa zinazohitajika kufikia alama za ubora wa bidhaa; na 30 wamepatiwa mafunzo ya kuongeza thamani mazao ya matunda na mboga mboga;

ii. Kwa kushirikiana na taasisi ya Technosave imeratibu mafunzo ya siku tatu kwa wakufunzi juu ya usafi na usalama (food safety) wa bidhaa za chakula ambapo jumla ya washiriki 22 (wanaume 9 na wanawake 13) kutoka Manispaa ya Mjini, ZBS, ZFDA, Idara ya Viwanda, SMIDA, TAHA, UWAMWIMA, Sekta ya kilimo, Maafisa wa Afya na wauza bidhaa Forodhani wameshiriki katika mafunzo hayo. Matokeo ya mashirikiano baina ya SMIDA na Technoserve yamepelekea kusainiwa kwa MoU baina ya SMIDA na Technoserve ambayo itaongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa SMIDA;

iii. Katika hatua za kuwaendeleza wajasiriamali vijana SMIDA imeandaa mashindano ya Ubunifu katika fani ya TEHAMA na mashine, ambapo wabunifu 22 wameshiriki kati yao wanaume 16 na wanawake 6. Hatua za kuwaendeleza baadhi ya wabunifu hao zimeanza kuchukuliwa kwa mbunifu wa majiko yanayotumia nishati inayotokana na mafuta yaliyokwishatumika (Wasted Oil). Aidha, majiko hayo yamefanyiwa uchunguzi na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na imethibitika kuwa yanaweza kutumika.

iv. Imemuwezesha mjasiriamali ZAIDAT PRODUCT ambae anazalisha bidhaa zinazotokana na mwani

kushiriki katika mashindano ya Ubora ya Kitaifa ya mwaka 2022, ambapo alipata tuzo ya ubora wa bidhaa zake kwa mwaka 2022

v. Imefanya matengenezo ya makubwa ya kituo cha mafunzo Kizimbani kupitia ufadhili wa KOICA, pamoja na Ununuzi wa mashine za uzalishaji wa bidhaa mbali mbali chini ya ufadhili wa UNIDO. Aidha, SMIDA imeendelea na juhudi za kuimarisha maeneo ya uzalishaji kwa wajasiriamali wenye viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya Kati kwa kuendeleza eneo la uzalishaji wa pamoja (Common Facilities) ambapo michoro kwa ajili ya ujenzi wa eneo hilo umekamilika.

## 5.2 WAKALA WA USAJILI BIASHARA NA MALI (BPRA)

***Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali***

**57. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Wakala wa Usajili Biashara na Mali (BPRA) yenye lengo la kufanya usajili wa biashara na mali ikijumuisha hati za mali bunifu pamoja na usajili wa nyaraka mbali mbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli za kibiashara Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 BPRA imepangiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi milioni 915.4** hadi kufikia tarehe 31 March 2023, imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 513.6** sawa na asilimia 56. Kati ya fedha hizo jumla ya **Shilingi milioni 442.4** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi milioni 71.23** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

58. **Mheshimiwa Spika,** BPRA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 1.15** kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato kwa huduma zinazotolewa. Katika kipindi cha Julai-Machi BPRA imekusanya **Shilingi bilioni 1.3** sawa na asilimia **111** zilizokusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

59. **Mheshimiwa Spika,** kupitia huduma ya Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali BPRA imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kufanya usajili wa Kampuni 1,121 Majina ya Biashara 1,802, Alama za biashara 1,160 na Nyaraka 5,798;

ii. Kutoa elimu kwa wananchi na wafanyabiashara mbalimbali juu ya ufahamu wa usajili wa biashara na mali kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

iii. Kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wafanyakazi wa BPRA. Wafanyakazi 2 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na 1 muda mfupi. Mfanyakazi 1 amepatiwa mafunzo ya shahada ya uzamili katika fani ya Procument and Supply Management Kwa Unguja na Pemba mfanyakazi 1 amepatiwa mafunzo ya stashahada ya Community Development katika Chuo cha Wete Institute of Academy Research and Consultancy na Mfanyakazi 1 mafunzo ya muda mfupi

ya ‘’Advance Course on Topical Intellectual Property Policy Issues ‘’ nchini Geneva, Switzerland;

iv. Kushiriki katika warsha ya dhana ya umiliki wa manufaa nchini Zambia na mkutano wa wadau juu ya sera ya taifa ya mali ubunifu (National Intellectual Property Policy) Zanzibar ambapo BPRA alikuwa mwenyeji wa mkutano huo akishirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia Mali bunifu Duniani (WIPO).

## 5.3 WAKALA WA VIPIMO ZANZIBAR (ZAWEMA)

***Utoaji Huduma ya Ulinganishi na Matumizi sahihi ya Vipimo***

**60. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) chini ya sheria namba 6 ya mwaka 2020 yenye lengo la kuhakikisha majibu ya vipimo katika miamala ya biashara yanafanyika kwa usahihi pamoja na kufanya uhakiki wa vipimo.

**61. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ZAWEMA ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 637.60** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 Wakala imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 162.64** sawa na asilimia **26** ya makadirio ya mwaka. Aidha ZAWEMA ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi milioni 391.04** kutokana na chanzo chake cha mapato,

hadi kufikia tarehe 31 Machi,2023 ZAWEMA imeweza kukusanya **Shilingi milioni 264.5** sawa na asilimia **67.7** ya makadirio ya mwaka na kuziingiza katika mfuko mkuu wa serikali.

62. **Mheshimiwa Spika,** kupitia huduma ya Ulinganishi na Matumizi sahihi ya Vipimo, ZAWEMA imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kufanya ukaguzi wa mizani za maduka 604, uhakiki wa Mita za mafuta 552 katika vituo vya mafuta, bohari na uwanja wa ndege, Matangi 49 na Magari 6 ya kusambazia mafuta, Tangi 1 la kuhifadhia mafuta, bidhaa 42 zilizofungashwa na mezani 1 kubwa ya kupimia magari; Pamoja na kuhakiki lita za mafuta 166,654,765.

ii. Kufanya ununuzi wa viti 10, meza 10, komputa 1, printer 1 na makabati 2 pamoja na kufanyika kwa kikao kimoja cha Bodi.

## 5.4 TUME YA USHINDANI HALALI WA KIBIASHARA NA KUMLINDA MTUMIAJI (ZFCC)

***Uimarishaji wa Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji***

63. **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji

(ZFCC) chini ya sheria namba 5 ya mwaka 2018 yenye lengo la kuhamasisha, kuimarisha na kulinda ushindani halali wa biashara na kumlinda mtumiaji hapa Zanzibar.

**64. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ZFCC ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 220.6** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 109.9** sawa na asilimia **50** ya makadirio ya mwaka. Aidha ZFCC ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi milioni 965.6** kutokana na vyanzo vyake vya mapato, hadi kufikia tarehe 31 Machi, ZFCC imeweza kukusanya **Shilingi milioni 341.5** sawa na asilimia **35** ambazo zimeingizwa katika mfuko mkuu wa serikali. Hali hii imetokana na upungufu wa vifaa vya kufanyia kazi.

**65. Mheshimiwa Spika,** kupitia huduma ya ***Uimarishaji wa Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji*** ZFCC imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Imepokea na kukamilisha maombi manne (4) ya Miungano ya Kampuni kati ya hayo mawili yaliwasilishwa na Kampuni ya Sanlam Allianz Africa Proprietary Limited ikiwa ni ombi la kuchukua asilimia 64.18 ya hisa za kampuni ya Sanlam Life Insurance (Tanzania) Limited na asilimia 51 ya hisa za kampuni ya Jubilee General Insurance Company of Tanzania Limited;

Vile vile, ombi la Kampuni ya HTT Infranco Limited

la kutaka kununua haki ya uendeshaji wa minara ishirini na moja (21) ya mawasiliano inayomilikiwa na Kampuni ya Viettel (Halotel) Tanzania PLC na ombi la Kampuni ya Brac Tanzania Finance Limited la kutaka kununua asilimia **99.9** ya hisa za Kampuni ya Brac Zanzibar Finance limited;

ii. Imekamilisha uandaaji wa Hadidu rejea (ToR) kwa ajili ya kuandaa mfumo wa kieletroniki utakaosaidia kubadilishana taarifa baina ya TRA, ZRA, ZIPA, BPRA na ZFCC.

iii. Imetoa uelewa wa sheria ya Tume ya Ushindani Halali wa Biashara Zanzibar katika Skuli ya Sekondari ya Biashara Zanzibar ambapo jumla ya walimu 37 na wanafunzi 228 wamepatiwa uelewa huo pamoja na kuandaa rasimu ya awali ya miongozo ya kufanya uchunguzi na uchambuzi wa miungano ya makampuni;

iv. Imeandaa rasimu ya awali ya kufanya uchunguzi katika soko na kuandaa miongozo ya kusimamia mienendo ya biashara inayokatazwa (restrictive business practices);

v. Imefanya ukaguzi wa maduka (Super Market) na maghala 960 kwa lengo la kubaini ubora/usalama na bei za bidhaa. Katika ukaguzi huo wafanyabiashara 131 waligundulika kukiuka bei elekezi kwa bidhaa zilizodhibitiwa na kutokuweka bei ya utambulisho wa bidhaa na Wafanyabiashara 30 walikutwa na bidhaa bandia zisizo salama kwa matumizi ya binaadamu na

imepokea malalamiko 5 ya Ushindani usio halali;

vi. Imefanya ukaguzi wa mikataba kumi na mbili (12) ya Kampuni ya Tanzania Commecial Bank (TCB) na kupatiwa vyeti.

### 5.5 BARAZA LA USHINDANI HALALI WA BIASHARA ZANZIBAR (ZFTC)

***Usikilizaji na Utoaji wa Maamuzi ya Rufaa za Ushindani zinazotokana na Mamlaka za Uthibiti***

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Baraza la Ushindani Halali wa Biashara Zanzibar (Zanzibar Fair Competition Tribunal - ZFCT), ambayo ni taasisi ya kisheria iliyoundwa ndani ya sheria namba 5 ya mwaka 2018 chini ya kifungu cha 26, yenye lengo la kutoa haki kupitia kusikiliza rufaa zinawasilishwa na wafanyabiashara au wazalishaji kutoka kwa Mamlaka za Udhibiti. Baraza hili ni chombo cha kuimarisha udhibiti wa vitendo vinavyokwenda kinyume na kuathiri ushindani wa biashara na kumlinda mtumiaji wa bidhaa na huduma ndani ya Zanzibar.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ZFCT ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 417.3** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 ZFCT imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 122.1** sawa na asilimia **37** ya makadirio ya mwaka. Kupitia huduma hii mambo yafuatayo yametekelezwa:

i. Imewapatia watendaji 11 mafunzo ya muda mfupi yanayohusiana na utunzaji wa majalada kielektroniki (E-office), Sekretarieti ya Bodi yanayotolewa na

IoDT, Stadi za uhudumu wa nyaraka, utunzaji wa siri za ofisi na maadili kwa watumishi wa Umma, maadili katika kuandaa na kutunza kumbukumbu na nyaraka za serikali kwa njia ya Tehama, utayarishaji wa Bajeti ili waweze kujua haki na wajibu wao utakaopelekea kufanya kazi kwa ufanisi na uweledi;

ii. Baraza limekamilisha uandaaji wa rasimu ya mkataba wa huduma, rasimu ya Mpango Mkakati na rasimu ya muundo wa utumishi;

iii. Kukamilika kwa kikao kimoja cha bodi ya Baraza pamoja na kufanyika kwa makongamano mawili Unguja na Pemba na vipindi 4 kwa redio na TV vya kuelimisha jamii juu ya kazi za Baraza.

## 5.6 BARAZA LA UDHIBITI WA MFUMO WA UTOAJI LESENI ZANZIBAR (BLRC)

***Usimamizi wa Mamlaka zinazotoa Leseni***

**68. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji Leseni (BLRC) chini ya sheria namba 13 ya mwaka 2013 yenye lengo la kudhibiti mfumo wa utoaji leseni na tozo kwa Mamlaka za Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 BLRC ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 441.7** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 BLRC imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 125.4** sawa na asilimia **28.3** ya makadirio ya mwaka. Aidha, BLRC ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi milioni 51.0**

kutokana na chanzo chake cha mapato, hadi kufikia tarehe 31 Machi, BLRC haikuweza kukusanya mapato kwa kipindi hiki kutokana na kutokukamilika kwa kanuni husika. Aidha kwa sasa kanuni hizo zimekamilika.

69. **Mheshimiwa Spika,** kupitia huduma ya Usimamizi wa Mamlaka zinazotoa Leseni BLRC imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:
   i. Kukamilika kwa mapitio ya leseni, vibali na ruhusa za ufanyaji Biashara kisekta ambapo katika shabaha yake ilijipangia kupitia sekta 16 pamoja na tozo zipatazo 400. Baraza limefanikiwa kupitia sekta nne ikiwemo Utalii, kilimo (na Misitu) na Elimu. Aidha, Baraza limepitia tozo 192 na Ripoti za mapitio hayo zimewasilishwa serikalini;
   ii. Kukamilika kwa mfumo wa kitaifa wa kielekroniki wa utoaji leseni (NOBS) ambao umezinduliwa kwa hatua ya majaribio na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda mwezi Machi, 2023. Vile vile, BLRC imezipatia taasisi 14 vifaa (computer) ambazo ni halmashauri 11 na idara 3 ili ziweze kutumia mfumo huu wa NOBS;
   iii. Kukamilika kwa tathmini ya mazingira ya Biashara Zanzibar kwa mwaka 2022 ambapo matokeo yanaonesha kwamba Zanzibar imeshika nafasi ya 92 kati ya nchi 191 iliyojilinganisha nazo kwa kupata alama 64.55 na nafasi ya nne (4) kwa nchi za visiwa. Kwa sasa Zanzibar imepiga hatua katika urahisi wa

ufanyaji biashara na kuingia katika kundi la nchi zenye mazingira mazuri ya biashara kwa sifa maalum (Most notable improvement business environment) kwa kutoka nafasi ya 155 hadi 92;

iv. Kufanyika ukaguzi wa Mamlaka 44 za utoaji leseni kwa kuangalia utekelezwaji wa miongozo inayotolewa na Baraza katika kuondosha urasimu kwenye ufanyaji Biashara Zanzibar. Katika ukaguzi huo Baraza limegundua kukosekana kwa baadhi ya kanuni na miongozo katika Mamlaka na uwezo mdogo wa kifedha ambao unasababisha kuchelewa kwa uanzishwaji wa mifumo ya kielektroniki.

## 5.7 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)

***Uandaaji wa Viwango na Tathmini ya Ubora***

70. **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) chini ya sheria namba 1 ya mwaka 2011 yenye lengo la kusimamia uanzishwaji na usimamizi wa viwango kwa huduma na bidhaa. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ZBS ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 1.37.** Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 1.04** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi milioni 326.90** kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 ZBS imeingiziwa jumla ya **Shilingi bilioni 1.28** sawa na asilimia **94** ya makadirio ya mwaka. Aidha ZBS ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi bilioni 1.65** kutokana na chanzo chake cha mapato, hadi kufikia tarehe 31

Machi,2023 ZBS imeweza kukusanya **Shilingi milioni 911.3** sawa na asilimia **55** kwa makadirio ya mwaka na kuziingiza katika mfuko mkuu wa serikali.

71. **Mheshimiwa Spika,** kupitia huduma ya ***Uandaaji wa Viwango na Tathmini ya Ubora*** ZBS imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

    i. Kuandaa na kuuza viwango 92, kati ya hivyo 41 vya bidhaa za chakula, 19 bidhaa za kemikali, 8 vya mazingira, 5 vya huduma za utalii, 7 bidhaa za umeme na elektoniki na 12 vya ujenzi. Aidha, jumla ya viwango 40 vya kemikali, mazingira, chakula, uhandisi ujenzi na uhandisi mitambo na vyombo vya moto.

    ii. Kutoa leseni 12 za matumizi ya alama ya ubora , leseni 7 Alama za Ubora kwa kutumia viwango vya Zanzibar **(ZBS Quality Mark)** na leseni 5 kwa mfumo wa kuthibitishwa kwa kutumia viwango visivyokuwa vya Zanzibar (Tested Product Certification);

    iii. Kufanya uchunguzi wa sampuli 509 na ripoti za sampuli 452 zimetolewa majibu, ambapo ripoti imeonesha sampuli 20 hazikukidhi mahitaji ya viwango husika;

    iv. Kukagua Shehena za bidhaa nyenginezo (General goods) ambapo shehena 1,253 zimekaguliwa kupitia mfumo wa ukaguzi nje ya nchi (PVoC) na Shehena 6,676 zimekaguliwa kupitia mfumo wa ndani ya nchi (DI) na kupatiwa vyeti vya ubora. Aidha, gari 3,132,

pikipiki 4,059, Shehena za mizigo 1,895 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, lita za mafuta ya nishati 146,673,958.

v. Kufanya ukaguzi katika bandari ya Mkoani na Wete, ukaguzi katika soko na ukaguzi katika maeneo ya uzalishaji na jumla ya Shehena 709, gari 31, pikipiki 446 zimekaguliwa;

vi. Kushiriki katika mikutano 20 inayohusiana na uandaaji wa viwango Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha kuwa matakwa ya wadau wa Zanzibar yanawasilishwa na kujumuishwa ipasavyo.

## 5.8 BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA (ZNBC)

***Uimarishaji wa Majadiliano ya Kibiashara Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi***

72. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Biashara la Taifa ni Jukwaa linaloweka pamoja Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa madhumuni ya kujadili changamoto za kibiashara na kuzitafutia utatuzi. Baraza hili hukutana chini ya Mwenyekiti wake Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kujumuisha wajumbe kutoka Sekta ya Umma ambao ni Mawaziri na wajumbe kutoka Sekta Binafsi ambao ni wakuu wa Taasisi za Sekta Binafsi wakiongozwa na Jumuiya ya Wafanyabiashara ya Zanzibar (ZNCC).

73. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022 – 2023 huduma ya Uimarishaji wa Mashirikiano baina ya sekta ya Umma na Sekta binafsi ambayo inatekelezwa na Baraza la Taifa la Biashara, ilipangiwa kutumia **TZS milioni 317.7** ikiwa ni ruzuku kwa ajili ya matumizi yake ya kawaida, hadi kufikia Machi 2023 Baraza lilipokea jumla ya **TZS 122.5** milioni sawa na asilimia **38.5.** Aidha, Baraza limepokea **TZS 25.1 milioni** kutoka kwa wahisani mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake.

74. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho Mkutano mmoja wa Baraza la Taifa la Biashara ulifanyika chini ya Mwenyekiti wake Dk. Hussein Ali Mwinyi, na kufuatiwa na Jukwaa la kumi na mbili la Biashara la Zanzibar. Katika mkutano huo hoja mbali mbali za wafanyabiashara zilijadiliwa na kupatiwa ufumbuzi. Hoja hizo zilihusiana na kuanzishwa kwa Fao la Ukosefu wa Ajira, kuanzishwa kwa mfumo wa One Stop Centre kwa ajili ya kurahisisha taratibu za utoaji wa mizigo bandarini, kuanzishwa kwa Mfuko wa Bima ya Afya wa Zanzibar na kuanzisha Muongozo wa Makubaliano ya Mauziano kwa njia ya mkopo baina ya muuzaji na mnunuzi wa bidhaa za kilimo zinazopelekwa katika mahoteli ya kitalii. Aidha, Kamati Tendaji ya Baraza ilikutana mara mbili kwa ajili ya kuandaa Mkutano huo wa baraza Pamoja na Jukwaa la Biashara.

75. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine Jukwaa la Biashara la kumi na mbili lilifanyika likiwa limebeba kauli

mbiu isemayo “Kukuza Uchumi Anuai katika kuimarisha maendeleo endelevu  na jumuishi”. Kero mbali mbali za wafanyabiashara zilijadiliwa zikiwemo; Uhaba wa mzunguko wa Dola ya Marekani , Taratibu za uingizaji mizigo kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar,Uboreshwaji wa huduma za kijamii katika sehemu za kitalii ikiwemo umeme, maji safi na salama, Udhibiti wa sauti kubwa zinazotokana na upigaji muziki pamoja na Ucheleweshwaji wa utowaji wa Makontena Bandarini.

76. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba changamoto zote zilizowasilishwa katika Jukwaa hilo zilitolewa maelekezo ya utekelezaji wake na Mwenyekiti wa Jukwaa hilo Dk. Hussein Ali Mwinyi ambae pia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na pia Wizara yangu kupitia Sekretarieti ya Baraza hilo itahakikisha inaratibu utekelezaji wa maazimio hayo ya Jukwaa la Biashara.

### 5.9 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

77. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Biashara la Taifa kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika (Corporate Strategic Plan) wa miaka mitano pamoja na mpango wa biashara wa miaka mitano 2021-2025. Kwa mwaka 2022/23 msimu wa karafuu umekuwa wa wastani ukilinganishwa na msimu wa mwaka 2021/2022 ambao

ulikuwa ni mkubwa. Utekelezaji wa mapato na matumizi kwa miezi tisa kuanzia Julai 2022 – Machi 2023 ni kama unavyoonekana hapa chini;

78. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miezi tisa Shirika lilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 87.5** kutoka katika vianzio vyake vya mapato vikiwemo; mauzo ya karafuu na mafuta ya mimea, mapato yanayotokana na majengo na mauzo yanayotokana na bidhaa za Tawi la ZSTC Dar es Salaam pamoja na mapato mengine. Hadi kufikia Machi 31, Shirika limeweza kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 77.4** sawa na asilimia **88** ya makadirio kwa mwaka. Shirika limeweza kukusanya mapato yake kama ifuatavyo: Mauzo ya karafuu tani 3,939.5; Mauzo ya Mafuta, **Shilingi milioni 243.5.** Kushuka kwa makusanyo hayo kumetokana na uzalishaji wa mafuta kiwandani kuwa ni mdogo kwa sababu ya kuharibika kwa mitambo mara kwa mara.

Aidha, Mapato ya Fedha za Majengo, Shirika limekusanya jumla ya **Shilingi milioni 309.4** ambazo ni sawa na asilimia **41** ya makadirio kwa miezi tisa. Kushuka kwa mapato hayo kumesababishwa na kuhama kwa baadhi ya wapangaji. Hata hivyo, Shirika linafuatilia madeni ambayo hayajalipwa na kutafuta wapangaji wengine.

79. **Mheshimiwa Spika,** Shirika katika kipindi cha Julai 2022 – Machi 2023 lilipanga kutumia jumla ya **Shilingi bilioni**

**85.7** kwa kazi za uendeshaji wa Shirika. Hadi kufikia Machi 31, Shirika limetumia jumla ya **Shilingi bilioni 61.3** sawa na asilimia **71** ya makadirio kwa miezi tisa. Mchanganuo wa matumizi hayo umegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo:

i. Uendelezaji na usimamizi wa zao la karafuu pamoja na Vifaa vya Vuno. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Shirika lilipanga kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni 74.6.** Hadi kufikia Machi 31 Shirika limetumia jumla ya **Shilingi bilioni 55.4** ambazo ni sawa na asilimia 74 ya makadirio kwa miezi tisa.

**80.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika lilipanga kununua tani 4,940 za karafuu kavu kwa gharama ya **Shilingi bilioni 69.1** ambapo bei ya kununulia karafuu iliyokadiriwa kuwa ni wastani wa **Shilingi 14,000** kwa kilo moja. Hadi kufikia Machi 2023, Shirika limenunua jumla ya tani 3,917.28 za karafuu kwa thamani ya **Shilingi bilioni 52.1** ambazo ni sawa na asilimia **75** ya makadirio kwa miezi tisa. Sababu kubwa ya kushuka kwa ununuzi wa karafuu umetokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamepelekea karafuu nyingi kununuliwa katika robo ya kwanza;

**81.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika lilipanga kununua makonyo tani 988 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.48.** hadi kufikia Machi 2023 Shirika limeweza kununua tani 771.3 za makonyo kwa thamani ya **Shilingi bilioni 1.15** manunuzi

haya ni sawa na asilimia **78** ya makadirio kwa kipindi cha miezi tisa. Kushuka kwa ununuzi huo umetokana na kupungua kwa uzalishaji wa karafuu.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika lilipanga kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni 1.4** katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2022 - Machi 2023) kwa ajili ya kuwalipa Wachukuzi pamoja na gharama za usafirishaji wa karafuu. Hadi kufikia Machi 31 Shirika limetumia kiasi cha **Shilingi bilioni 1.9** ambazo ni sawa na asilimia 142 ya makadirio kwa kipindi cha miezi tisa; Aidha Shirika limefanikiwa kununua magunia, majamvi, nyuzi za katani na pishi kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.3** sawa na asilimia 86 ya makadirio ya 1.5 kwa kipindi cha miezi tisa. Vile vile, Shirika limetoa **Shilingi milioni 25.2** kwa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya Mikarafuu pamoja na kulipia **Shilingi milioni 370.6** kwa ajili ya kugharamia Kikosi Kazi cha kuzuwia magendo.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Kuhusu Uendeshaji wa Tawi la ZSTC Dar es Salaam, Shirika la Biashara Zanzibar Tawi la ZSTC Dar es Salaam lilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi milioni 513.3** katika mauzo ya bidhaa zake. Hadi kufikia Machi 2023 Tawi limekusanya jumla ya **Shilingi milioni 423.9** sawa na asilimia **83** ya makadirio kwa kipindi cha miezi tisa. Aidha, kwa upande wa matumizi Tawi lilikadiria kutumia **Shilingi milioni 445.0.** Hadi kufikia Machi 2023, Tawi limetumia kiasi cha **Shilingi milioni 443.7** ambazo

ni sawa na asilimia **100** ya makadirio kwa kipindi cha miezi tisa;

84. **Mheshimiwa Spika,** Kuhusu Kuimarisha Vitega Uchumi vya Shirika, Shirika limefanya uimarishaji wa Vitega Uchumi vyake ambavyo ni pamoja kujenga Jengo lake liliopo Madungu Pemba kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.3** ambayo ni malipo ya Mkandarasi na **Shilingi milioni 86.6** kwa ajili ya kumlipa Mshauri elekezi wa kulisimamia Jengo hilo. Aidha ujenzi wa jengo hilo umefikia asilimia 78 ya kazi;

85. **Mheshimiwa Spika,** kuhusu Kuimarisha Mfumo wa Masoko wa Shirika, Shirika limeweza kutumia jumla ya **Shilingi milioni 44.6** kwa ajili ya matangazo ya biashara, gharama za maonesho na gharama za Utafiti wa Masoko. Aidha, kuhusu Uendelezaji wa Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo na Arki za Mimea, Kiwanda kilipanga kutumia kiasi cha **Shilingi milioni. 493.0,** hadi kufikia Machi 31 Kiwanda kimetumia kiasi ch**a Shilingi milioni 221.7** sawa na asilimia **45** ya makadirio kwa kipindi cha miezi tisa.

## 5.10 KAMPUNI YA MWANI ZANZIBAR (ZASCO)

86. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya mwani imeanzishwa na serikali kwa lengo la kusimamia na kuendeleza zao la mwani hapa Zanzibar. Kampuni hii imeundwa kwa ubia wa taasisi za serikali. Kwa 2022 –2023 Kampuni ilipanga

kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 9.389** hadi kufikia Machi 2023, Kampuni imetumia jumla ya **Shilingi bilioni 5.674** sawa na asilimia **60.4** ya makadirio ya mwaka. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Kampuni imeweza kutekeleza shughuli zake kulingana na Mpango kazi wake kama ifuatavyo:

i. Kununua na kuuza mwani: Hadi kufikia Machi 31, Kampuni ya ZASCO ilifanikiwa kununua wastani wa tani 1,236 za mwani aina ya Ulva; mwani huo ulinunuliwa kwa bei ya TZS. 800 kwa kilo 1. Aidha, wastani wa tani 109 za mwani aina ya "Spinosum" kwa bei ya TZS. 1,000 badala ya 700 kwa kilo 1. Kadhalika, wastani wa tani 5.3 za mwani aina ya "Cottonii" zimenunuliwa kwa bei ya TZS 2,100 badala ya 1,800 kwa kilo 1. Katika hatua nyengine, Kampuni imefanikiwa kuuza wastani wa tani 500 za mwani wa Ulva. Jumla ya fedha zilizopatikana kutokana na mauzo hayo ni shillingi milioni 603.78;

ii. Kujenga Kiwanda cha Kusarifu zao la Mwani: Kampuni imeendelea na ujenzi wa kiwanda hicho kwa ufanisi. Ujenzi huo unahusisha ujenzi wa uzio wa eneo lote la kiwanda, jengo kuu la kiwanda na ghala. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kwamba eneo lote la kiwanda limeshazungushwa ukuta. Ujenzi wa jengo kuu la kiwanda umefikia hatua ya kunyanyua vyuma na kuanza maandalizi ya kuezeka. Aidha,

Ujenzi wa ghala umefikia hatua ya kuezeka kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa fedha;

iii. Kuandaa Mpango Mkakati wa Kampuni na Mpango wa Biashara wa Kampuni: Kampuni imefanikiwa kuandaa rasimu ya Mpango Mkakati na Mpango wa Biashara wa Kampuni kwa miaka mitano ijayo kuanzia mwaka 2023 hadi 2027. Mipango hiyo inasubiri kujadiliwa katika ngazi ya uongozi ya Kampuni kwa hatua zaidi;

iv. Kuwapatia vifaa vya kulimia mwani wakulima wa mwani. Vikundi 57 vimepatiwa vifaa vya kulimia mwani vikiwemo taitai, kamba mm 4 na kamba mm 10. Tayari vifaa hivyo vimeshaanza kutumika;

v. Kuendesha vikao vya Wakurugenzi wa Mwanzo wa Kampuni: Vikao hivyo vilijadili mambo mbali mbali yenye mnasaba na uendeshaji wa Kampuni. Miongoni mwa mambo hayo ni kupitisha bajeti ya Kampuni, kujadili na kupitisha miongozo ya Kampuni na kujadili utekelezaji wa shughuli za Kampuni.

## 6. MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024

### 6.1 *Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2023/2024*

**87. Mheshimiwa Spika,** Katika kutayarisha Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imezingatia nyenzo muhimu

ambazo ni; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, hotuba mbali mbali na ahadi za Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizozitoa kipindi cha kampeni ya mwaka 2020, maono ya Baraza la Wawakilishi, Ukomo wa Rasilimali fedha uliowekwa kwa Wizara na Miongozo mbalimbali ya Kisera na kisheria inayosimamiwa na Wizara.

88. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kutekeleza vipaumbele katika maeneo makuu matatu (3) ambayo vinavyolenga kuimarisha Sekta ya viwanda, Kuimarisha Biashara na Kutafuta Masoko pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na utoaji huduma. Maeneo hayo ya vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo:

**Sekta ya Viwanda:**

89. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza sekta viwanda, Wizara imekusudia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Kuyaendeleza Maeneo ya Viwanda, Wizara inatarajia kuendelea kuimarisha maeneo ya Viwanda ya Dunga na Chamanangwe kwa kuyazungushia hifadhi ya ukuta (boundry walls), kujenga majengo ya viwanda

(prefabricated steel industrial sheds), kukamilisha miundombinu ya maji na umeme pamoja na kutengeneza barabara za ndani. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imepanga kukamilisha kazi za kulipima eneo la viwanda Pangatupu pamoja na kuandaa matumizi ya ardhi (detailed master plan) ya eneo hilo;

ii. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kukuza Vitega uchumi ZIPA itaendeleza juhudi za kutafuta wawekezaji ili lengo la kuanzishwa kwa maeneo hayo tengefu ya kukuza uchumi wa viwanda kwa kutoa ajira, kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato na kupunguza utegemezi wa kuagiza bidhaa kutoka nje liweze kufikiwa; na

iii. Kuanzisha Mfumo wa kusajili na kutoa leseni za Taifa za Viwanda kwa kushirikiana na Wakala wa Usajili wa Biashara na leseni (BRELA). Suala la kusajili na kutoa leseni za viwanda ni la Muungano hivyo linatekelezwa na BRELA kwa miaka mingi. Wizara imeanza mazungumzo na BRELA ili tuweze kusajili na kutoa leseni za viwanda kwa upande wa Zanzibar.

**Kuimarisha Biashara na Kutafuta Masoko:**

**90. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Biashara, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. **Kuendeleza Ujenzi kwenye eneo la maonesho ya kibiashara Nyamanzi:** Wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kumalizia ujenzi wa Ukuta, kuweka miundombinu kwa ajili ya kuwa na eneo la kudumu la maonesho ya Biashara. Aidha, Wizara imepanga kununua na kusimamisha vifaa vya kufanyia maonesho ikiwemo magazebo, Mashamiana madogo na kuweka samani ili kufanikisha maonesho katika eneo la Nyamanzi.

ii. **Kuratibu ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (Convention Centre):** Wizara itaendelea na juhudi za kutafuta wadau wenye masharti nafuu ili kushirikiana katika ujenzi wa kituo hiki.

iii. **Kujenga Vituo Jumuishi kwa ajili ya Urasimishaji Biashara:** Wizara katika kuendelea na kazi ya urasimishaji Biashara Zanzibar,kwa kipindi cha 2023/2024 itajenga vituo viwili vya urasimishaji biashara, ambapo kimoja kitajengwa Pemba (Bopwe) na chengine Unguja (Tunguu) ambapo taratibu za kuyapata maeneo hayo tayari zimeanza.

iv. **Kuandaa na Kuratibu Misafara ya kibiashara ndani na nje ya nchi (Trade Mission):** Kwa mwaka 2023/24, Wizara imepanga kuandaa na kuratibu misafara miwili ya kibiashara.

**Kuboresha Mazingira ya ufanyaji biashara na huduma**

**91. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Mazingira ya ufanyaji Biashara, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Kukamilisha mfumo wa Usajili na Malipo (Appeal Filling System), Wizara kupitia ZFCT kwa mwaka 2023/2024 imelenga kuanza kutumia mfumo kwa wadau wa Baraza ili kuweza kukata mashauri ya rufaa, kutuma nyaraka pamoja na viambatanisho vinavyohitajika ili kuweza kuendesha mashauri pamoja na kuwarahisisha malipo yanayohusiana na ukataji wa mashauri. Mfumo huo unalenga kurahisisha mchakato mzima wa ukataji wa rufaa kwa kupunguza muda na usumbufu pamoja na urasimu.

ii. Kuimarisha Tume ya Ushindani Halali wa Biashara; Wizara inatarajia kuifanyia marekebisho ya Sheria namba 5 ya mwaka 2018 ili kuyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wake. Aidha, kutafuta eneo la ujenzi wa ofisi kwa upande wa Pemba.

iii. Kuanza taratibu za ujenzi wa ofisi za Baraza la Udhibiti wa Mifumo ya Utoaji Leseni (BLRC), ili kuhakikisha watendaji wa BLRC wanapata mazingira mazuri ya kufanyia kazi pamoja na kutoa huduma kwa wafanyabishara.

iv. Kufanya mapitio ya Kanuni 50 za Mamlaka za Udhibiti na Usimamizi pamoja na kuendelea kusimamia mfumo wa NOBS ili Mamlaka zote za SMZ na SMT ziweze kutumia mfumo huu.

v. Kufanya Tafiti katika masuala ya biashara na viwanda, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa maendeleo ili kuhakikisha Sekta hizi zinazidi kukua na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa. Tafiti hizo zitalenga maeneo ya ushindani wa kibiashara, malighafi zinazopatikana ndani kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda na mazingira ya kibiashara.

vi. Kuweka mazingira mazuri ya wafanyakazi kwa kuandaa mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu pamoja na kuwapatia wafanyakazi nyenzo za ufanyaji kazi ili kuweza kutoa huduma zinazokidhi malengo katika sekta ya Biashara na Viwanda nchini.

vii. Kuratibu na kuandaa makongamano ya kibiashara baina ya Serikali na Binafsi (PPD), kupitia Baraza la Taifa la Biashara litatekeleza kipaumbele kwa kuibua changamoto zinazokabili ufanyaji biashara na kutafuta ufumbuzi ikiwemo kufanyia mabadiliko ya mfumo wa ufanyaji Baraza. Kipaumbele hiki kitaendana na mapitio ya sheria ya Baraza.

viii. Kuandaa eneo la maabara pamoja na kununua vifaa vya kupimia mita za maji kuhakikisha inajenga maabara na kununua vifaa vitakavyotumika kupima mita za maji. Aidha, Wizara kupitia ZAWEMA itaandaa kanuni kwa ajili ya upimaji wa mita za maji. Vile vile, Wizara imepanga kuandaa kanuni ya upimaji wa bidhaa zilizofungashwa ambapo kazi hii ya upimaji tayari imeanza.

ix. Kufanya Mapitio ya Sheria ya Nyaraka kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA), ambapo imepanga kufanya mapitio ya Sheria ya Nyaraka ya Mwaka 1919 pamoja na kukamilisha sheria ya Ubia na sheria ya Ufilisi ambazo zimepitwa na wakati ili iendane na mabadiliko yaliyopo.

x. Kuandaa Sera ya Taifa ya Zanzibar ya Mali Ubunifu (Intellectual Property – IP Policy kupitia Wakala wa Usajili Biashara na Mali kwa kushirikiana Shirika la Kimataifa la mali bunifu (WIPO) imepanga kuandaa sera hiyo katika kipindi cha 2023-2024.

xi. Kutoa uelewa kwa wafanyabiashara na vikundi vya wajasiriamali katika masuala ya urasimishaji, usajili na taratibu nyingine za kibiashara.

### Kuendeleza Taasisi ya Viwango

**92. Mheshimiwa Spika**, Katika kuendeleza Taasisi ya Viwango, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Uimarishaji wa Taasisi kwa kupata Ithibati ya Maabara (Accreditation), Wizara imepanga kuimarisha Taasisi ya Viwango (ZBS) na kupata Ithibati (Accreditation) ya Maabara mbili kwa mwaka 2023/2024 ambazo ni Maabara ya chakula na Maabara ya Mikrobiolojia;

ii. Kuimarisha huduma za udhibiti ubora ndani ya Taasisi na maabara katika maabara za Kemikali, Umeme na Maabara ya Ugezi pamoja na jengo lake.

iii. Wizara itaongeza juhudi za kutoa uelewa na uhamasishaji kwa wajasiriamali na wazalishaji kupata Alama ya Ubora ya ZBS. Tunatarajia jumla ya wajasiriamali 130 watapata alama za ubora, kati ya hao 30 kwa ufadhili wa Taasisi ya Viwango (ZBS) na wengine 100 watapata unafuu wa asilimia 50 ya gharama.

iv. Kukamilisha kituo cha ukaguzi wa magari na pikipiki katika eneo lililopo mkabala na ofisi za ZBS – Maruhubi ambacho kitakuwa na uwezo wa kukagua vyombo vya moto 300 kwa siku.

### Kuendeleza Shughuli za Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)

**93. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Biashara, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Ununuzi wa Karafuu na Makonyo, Wizara kupitia Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) imepanga kununua tani 4,600 za karafuu kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kwa gharama ya shilingi bilioni 63.2 na Makonyo tani 800 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.2;

ii. Kuongeza uzalishaji katika mafuta ya mimea unaongezeka kutoka tani 22 hadi tani 34.1 kwa mwaka 2023/2024 kwa kununua mtambo ambao utafungwa katika mashamba;

iii. Kuimarisha Vitega Uchumi vya Shirika ikiwa jumla ya shilingi bilioni 4.0 zimetengwa ili Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Madungu, ujenzi wa nyumba ya Malindi kwa ajili ya kuikodisha pamoja na utanuzi wa Ofisi ya Maisara.

### Kampuni ya Mwani (Zanzibar Seaweed Company Ltd)

**94. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Kampuni yaMwani (ZASCO) imeweka vipaumbele vifuatavyo:

i. Kumalizia ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu zao la mwani ambao unaendelea katika eneo la Chamanangwe Pemba kwa kusarifu mwani aina ya “Spinosum” na “Cottonii” ambao unatarajia kuzalisha “carrageeenan”. Aidha, ZASCO inatarajia kuongeza ununuzi wa mwani kufikia tani 4,500 (Spinosum tani 4,000 na Cottonii 500) kutoka tani 112.

ii. Kampuni inatarajia kuanza ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani aina ya Ulva, kiwanda hicho kinatarajiwa kujengwa Dunga Unguja kwa njia ya ubia baina ya ZASCO na wawekezaji. Kwa mwaka 2023/24 kampuni inatarajia kununua tani 6,000 za mwani aina hii ya Ulva kutoka tani 1,234.

### 6.2 Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2023/2024

**95. Mheshimiwa Spika** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2023/24 imepangiwa kutumia Jumla ya **shilingi bilioni 35.952.** Kati ya fedha hizo Jumla **shilingi bilioni 1.646,** ikiwa ni Matumizi ya kazi za kawaida na Mishahara **shilingi bilioni 4.304.** Aidha, **shilingi bilioni 28.417** zimetengwa kwa kazi za Maendeleo kwa programu ya kuendeleza Viwanda na biashara na ukuzaji masoko. Aidha, Wizara imepangiwa ruzuku ya **shilingi bilioni 1.584** kwa taasisi zake.

96. **Mheshimwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/24 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo ambayo ni mradi wa kuendeleza maeneo tengefu ya viwanda katika program ya Viwanda na kuendeleza kituo cha mikutano na eneo la maonesho ya kimataifa katika program ya biashara na ukuzaji masoko.

97. **Mheshimwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara Biashara na Maendeleo ya Viwanda itatekeleza program kuu tatu (3). Programu kuu hizo ni programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara; programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali; na programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara.

98. **Mheshimwa Spika**, Katika programu kuu ya uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda imegawika katika Programu ndogo tatu kwa mujibu wa huduma ambazo inazitoa. Program hizo ndogo ni Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Biashara na Viwanda; Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara; na Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba. Program hii imepangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 4.053.**

99. **Mheshimwa Spika,** Katika Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ambayo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ina jukumu la kutoa huduma

ya usimamizi wa rasilimali watu na huduma za kiofisi kwa ujumla pamoja na ununuzi wa vifaa. Ili kutekeleza majukumu yake, program hii ndogo imepangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 2.582** kwa mwaka wa fedha 2023/ 2024.

100. **Mheshimwa Spika**, kwa upande wa program ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ambayo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, ina jukumu la uandaaji na uibuaji wa sera na tafiti za Wizara, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Wizara pamoja na usimamizi wa takwimu za Biashara na Viwanda. Katika kutekeleza huduma hizo, programu ndogo ya uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti imepangiwa matumizi ya **shilingi milioni 570.499** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

101. **Mheshimwa Spika,** Program ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ambayo inaratibu shughuli za uendeshaji wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa upande wa Pemba imepangiwa matumizi ya **shilingi milioni 899.991** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

102. **Mheshimwa Spika,** katika program kuu ya pili ambayo ni Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali imegawika katika Programu ndogo mbili kwa mujibu wa huduma ambazo inazitoa. Program hizo ndogo ni Ukuzaji Viwanda

na Maendeleo ya Ujasiriamali. Katika kutekeleza shughuli za program hii imepangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 26.405.**

103. **Mheshimwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda itakuwa na jukumu la kutoa huduma ya Uimarishaji wa Sekta ya Viwanda, Uratibu na utekelezaji wa Sera ya MSME's na Ukuzaji wa MSME's. Ili kutekeleza programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 26.394** kwa mwaka 2023/2024.

104. **Mheshimwa Spika,** kwa upande wa programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ambayo ina jukumu la kutoa kuwakuza na kuwaendeleza wajasiriamali, Ili kutekeleza programu hii ndogo imetengewa **shilingi million 11.320** kwa mwaka 2023/2024.

105. **Mheshimwa Spika,** Programu kuu ya tatu itakayotekelezwa na Wizara kwa mwaka 2023/2024 ni Ukuzaji na Uendelezaji Biashara. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imegawanyika katika Programu ndogo tatu (3) ambazo ni Ukuzaji masoko na usafirishaji; uwezeshaji biashara na utengamano wa kibiashara. Ili kutekeleza huduma zilizopangwa katika Programu kuu hii ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara kwa mwaka 2023/2024, imepangiwa jumla ya **shilingi bilioni 5.493.**

106. **Mheshimwa Spika** Programu ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji itakuwa na jukumu la kutoa huduma ya kuongeza fursa za masoko kwa bidhaa za Zanzibar pamoja na urahisishaji biashara ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara. Ili kutekeleza majukumu hayo, programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji imetengewa **shilingi bilioni 3.806** kwa mwaka 2023/2024.

107. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa programu ndogo ya Uwezeshaji Biashara itakuwa na jukumu la kuimarishaji wa mazingira mazuri ya biashara, kuimarisha ushindani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji pamoja na kuondoa changamoto za ufanyaji biashara Zanzibar. Ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara, Wakala wa Vipimo, Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Baraza la Taifa la Biashara, Baraza la Ushindani, na Baraza la Mfumo wa Utoaji Leseni. Ili kutekeleza jukumu hili imepangiwa jumla ya **shilingi bilioni 1.647** kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

108. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utengamano wa Kibiashara wenye jukumu la kuimarisha biashara huria inayopelekea upanuzi wa sokona kuongeza biashara baina ya nchi na nchi utasimamiwa na Idara ya Biashara. Ili kutekeleza Shughuli zilizopangwa program hii ndogo imepangiwa jumla ya **shilingi milioni 39.920**.

## 7. MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024:

### 7.1 Mapato ya Serikali

109. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara yangu imepangiwa kukusanya jumla ya **shilingi Billioni 1.750.** Mapato hayo ukilinganisha na makusanyo ya mwaka 2022/2023 yamepungua kwa Jumla ya **shilingi Billioni 2.848** hii imesababishwa na maamuzi ya kujitegemea katika utendeji wa Taasisi ya Viwango Zanzibar na Wakala wa Usajili Biashara. Mapato hayo yatakusanywa kutoka vianzio vifuatavyo kama inavyoonekana katika **Jadweli Namba 1: -**

**Jadweli Namba 1:**
**Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023 – 2024**

| KIFUNGU | MAELEZO | MAKADIRIO |
|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo, Zanzibar** | **563,644,000** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizani na Vipimo | 563,644,000 |
| | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani halali Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **957,850,000** |
| 1422077 | Malipo ya Kazi za Biashara | 957,850,000 |
| | | |
| **R0105** | **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | **16,896,000** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 16,896,000 |
| | | |
| **R0110** | **Baraza la Leseni (BLRC)** | **63,953,000** |
| 1422118 | Ada ya usimamizi wa Mamlaka za Leseni | 63,953,000 |
| | | |
| **R0104** | **Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM)** | **99,933,000** |
| 1422038 | Ada ya vibali vya usafirishaji | 99,933 ,000 |
| | | |
| **R0101** | **Afisi Kuu Pemba** | **47,724,000** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizani na Vipimo | 39,717,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 8,007,000 |
| | **Jumla** | **1,750,000,000** |

### 7.2 Matumizi

**110. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi na ili Wizara yangu iweze kutekeleza programu zake ilizojiwekea kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya jumla ya **shilingi bilioni 35.952** kwa programu tatu (3) kama inavyoonekana katika **Jadweli Namba 2.**

**Jadweli Namba 2 :**
**Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2023/2024**

| KIFUNGU | Programu Kuu/ Programu Ndogo | Makadirio '000' |
|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda** | **4,053,416** |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 2,582,926 |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | 570,499 |
| SR010103 | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 899,992 |
| | | |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **26,405,044** |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 26,393,724 |
| SR010202 | Maendeleo ya Ujasiriamali | 11,320 |

| | | |
|---|---|---|
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **5,493,540** |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 3,806,374 |
| SR010302 | Uwezeshaji wa Biashara | 1,647,246 |
| SR010303 | Utengamano wa Biashara | 39,920 |
| **JUMLA KUU** | | **35,952,000** |

Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya *Viwanda Zanzibar*.

## 8. SHUKRANI:

111. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Wizara yaliyopatikana ni matokeo ya mashirikiano makubwa ya Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti. Shukrani zangu pia ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii wajumbe na Makatibu wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na miongozo waliyoitoa katika mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yangu na hatimae kuridhia mapendekezo haya yawasilishwe katika Baraza hili.

112. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imepata ushirikiano kutoka kwa wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu, Hivyo, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Jumuiya ya Ulaya (EU), USAID, Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa

la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Shirika la Kimataifa la Tasnia ya Malibunifu (WIPO), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), TradeMark Africa (TMA), Benki ya Dunia (World Bank), Shirika la Biashara Duniani (WTO), TANTRADE, Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania (COSTECH), REPOA, Zanzibar Seaweed Cluster Initiative (Zasci), Milele Foundation, Jumuiya za Wafanyabiashara, Zanzibar (ZNCC), Taasisi mbalimbali zilizotusaidia kufanikisha tamasha la biashara la 9 pamoja na Wafanyabiashara wote wakubwa , wadogo na Wawekezaji wa Viwanda.

## 9. HITIMISHO:

**113. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuimarisha mahusiano katika uwekezaji wa viwanda, kutafuta masoko na tafiti zinazohusu Sekta za Biashara na Viwanda.

**114. Mheshimiwa Spika**, napenda nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali, ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja

## 10. VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho Namba 1**

**Mapato ya Wizara kwa kipindi Julai 2022 -Machi 2023**

| Kifungu | Maelezo | Makadirio Julai-Machi)2022/2023 | Makusanyo (Julai-Machi 2022/2023) | Asilimia ya Makusanyo |
|---|---|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo, Zanzibar** | **251,985,000** | **238,783,442** | **95%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo | 251,985,000 | 238,783,442 | 95% |
| | | | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani halali Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **704,580,000** | **341,506,000** | **48%** |
| 1422077 | Malipo ya Kazi za Biashara | 704,580,000 | 341,506,000 | 48% |
| | | | | |
| **R0105** | **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | **95,665,500** | **500,000** | **1%** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 95,665,500 | 500,000 | 1% |
| | | | | |
| **R0106** | **Wakala wa Usajili Biashara na Mali** | **837,442,277** | **553,255,613** | **66%** |
| 1146002 | Ada ya Utunzaji Urithi | 2,626,277 | 1,076,574 | 41% |
| 1422030 | Alama za Biashara | 367,293,000 | 150,498,273 | 41% |
| 1422031 | Uandikishaji wa Makampuni | 316,492,000 | 230,177,971 | 73% |
| 1422032 | Uandikishaji Majina ya Biashara | 92,007,000 | 38,670,595 | 42% |
| 1422034 | Ujira wa kutengeneza Nyaraka | 59,024,000 | 132,832,200 | 225% |
| | | | | |
| **R0107** | **Taasisi ya Viwango Zanzibar** | **1,300,554,366** | **911,336,000** | **70%** |
| 1112008 | Malipo yatokanayo na Usimamizi wa Viwango | 1,300,554,366 | 911,336,000 | 70% |
| | | | | |
| **R0110** | **Baraza la Leseni (BLRC)** | **51,000,000** | **-** | **-** |
| 1422118 | Ada ya usimamizi wa | 51,000,000 | - | - |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mamlaka za Leseni | | | |
| | | | | |
| **R0104** | **Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM)** | **125,294,000** | **62,086,762** | **50%** |
| 1422038 | Ada ya vibali vya usafirishaji | 125,294,000 | 62,086,762 | 50% |
| | | | | |
| **R0101** | **Afisi Kuu Pemba** | **102,516,000** | **73,930,501** | **72%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo | 49,205,000 | 25,759,201 | 52% |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 26,331,000 | - | 0% |
| 1422034 | Ujira wa kutengeza Nyaraka | 26,980,000 | 48,171,300 | 179% |
| **Jumla** | | **3,469,037,143** | **2,181,398,318** | **63%** |
| | Stamp Duty (BPRA) | - | 694,519,210 | - |
| **JUMLA KUU** | | **3,469,037,143** | **2,875,917,528** | **83%** |

Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda,2023

## Kiambatanisho Namba 2


# MATUMIZI YA PROGRAMU KWA JULAI 2022- MACHI 2023

| KIFUNGU | PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA KWA MWAKA | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA KWA MIEZI 9 | FEDHA ZILIZPATIKANA KWA MIEZI 9 | ASILIMIA YA KILICHOPATIKANA KWA MIEZI 9 |
|---|---|---|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na Uratibu wa Wizara** | **2,977,527,000** | **2,340,711,002** | **2,325,671,159** | **99%** |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 1,710,045,491 | 1,310,984,121 | 1,339,316,023 | 102% |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | 522,113,509 | 439,700,881 | 341,125,356 | 78% |
| SR010103 | Uratibu wa Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 745,368,000 | 590,026,000 | 645,229,780 | 109% |
| | | | | | |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **13,701,922,000** | **12,069,955,350** | **1,528,400,502** | **13%** |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 3,276,292,000 | 3,115,743,500 | 1,228,129,022 | 39% |
| SR010202 | Maendeleo ya wajasiriamali | 10,425,630,000 | 8,954,211,850 | 300,271,480 | 3% |
| | | | | | |
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendeleza** | **9,685,951,000** | **8,009,258,489** | **4,466,444,484** | **46%** |

| | ji wa **Biashara** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| SR010 301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 4,955,451,0 00 | 4,199,715,5 00 | 1,004,693, 535 | 24% |
| SR010 302 | Uwezeshaji wa Biashara | 4,625,060,0 00 | 3,726,802,9 89 | 3,454,305, 949 | 93% |
| SR010 303 | Utengaman o wa Biashara | 105,440,000 | 82,740,000 | 7,445,000 | 9% |
| **JUMLA YA KIFUNGU R01** | | **26,365,40 0,000** | **22,419,92 4,841** | **8,320,51 6,145** | **37%** |


## Kiambatanisho Namba 3

### Mchoro Nambari 2: Mwenendo wa Biashara Zanzibar (2018– 2022)



**Kiambatanisho Namba 4**

**Mchoro Na 1: Uagiziaji na Usafirishaji kwa mwaka 2022 kwa TZS "000"**



**Kiambatanisho Namba 5**

**Wastani wa Uingizaji wa Chakula Muhimu**
**<u>katika Soko la Zanzibar 2022/2023 (Tani):</u>**

| | **Bidhaa/tani** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Mchele** | **Sukari** | **Unga wa ngano** | **Mafuta ya kula** |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka nje ya nchi (Jul 2022- Machi, 2023) | 99,400 | 4,302 | 1,700 | 84,839 |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka T. Bara | 571 | - | 3,987 | - |
| Bidhaa Zilizozalishwa nchini | - | 6,796 | 41,720 | - |
| **Jumla ya Bidhaa** | **99,971** | **10,545** | **47,407** | **84,839** |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2022***

**Kiambatanisho Namba 6.**

## Wastani wa Bei za Reja Reja (KG) za Chakula Muhimu Katika Soko la Zanzibar, 2022/2023.

| BIDHAA/kg | WASTANI WA BEI (TSH) ZA REJA REJA / KG | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JUL | AUG | SEPT | OCT | NOV | DEC | JAN | FEB | MAR |
| Mchele wa Basmati | 4,000 | 4,000 | 4,000 | 4,000 | 4,500 | 4,500 | 4,500 | 4,000-4,500 | 4,000-4,500 |
| Mchele aina nyengine | 1,700 | 1,800 | 1,800 | 1,800 | 1,800 | 2,000-2,200 | 2,000-2,200 | 2,000 | 1,800-2,000 |
| Mchele wa Mbeya/kg | 2,400 - 3,000 | 2,500 - 3,000 | 2,600-3,000 | 2,600-3,000 | 3,000-4,500 | 3,000-4,500 | 3,000-4,600 | 3,000-4,600 | 3,000-4,600 |
| Unga wa ngano /kg | 1,800 | 1,800 - 2,000 | 1,800-2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 2,000 | 1,900-2,000 | 1,900 - 2,000 |
| Sukari /kg | 2,200 - 2,500 | 2,200 - 2,500 | 2,200-2,500 | 2,200-2,500 | 2,200-2,500 | 2,200-2,500 | 2,200 – 2,500 | 2,400 – 2,500 | 2,400 – 2,500 |

*Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2023*